# AGANO LA MAOMBI
## *Kwa Watoto*

| | |
|---|---|
| **NEEMA** | Baba Mwenyezi Mungu, nakushukuru kwa kunipenda na kunifanya mmoja ya watoto wako. |
| **UPENDO** | Nisaidie nikupende na nikutii. |
| **HURUMA** | Nisaidie nipende wenzangu unavyonipenda. |
| **KUTUBU** | Natubu dhambi zangu. Nitakase niwe msafi. |
| **KUSIFU** | Nitakutukuza na moyo wangu wote! |
| **KUJITOLEA** | Yesu nataka kukufuata.Nibadilishe vyovyote utakavyo. |
| **KUTEGEMEA** | Nijaze na Roho Mtakatifu, nataka kujua mipango yako kwangu |
| **USHAWISHI** | Nifanye mtumishi wako wa neema, ukweli na haki. |
| **UFUASI** | Nitumie kwa utukufu wako niweze kualika wengine wakufuate |
| **MAMLAKA** | Katika jina la Yesu naomba. Amina. |

**KUMFUATA YESU PAMOJA.**

*theprayercovenant.org/children*

# MISTARI YA BIBILIA YA KUKARIRI

**Fumbo la Kondoo Aliyepotea · Luka 15:1-7** | Tazameni jinsi Baba alivyotupenda mno, hata tukaitwa watoto wa Mungu! –1Yohana 3:1

**Hadithi ya Abrahamu · Kitabu cha Mwanzo 12:1-5** | Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote na kwa akili zako zote. Hii ndio amri kuu, tena ni ya kwanza. –Mathayo 22:37-38

**Msamaria Mwema · Luka 10:25-37** | Amri yangu ni hii, pendaneni kama nilivyowapenda. –Yohana 15:12

**Fumbo la Mfanyakazi Asiyesamehea · Mathayo 18:21-35** | Nioshe kabisa kutoka hatia yangu na unitakase dhambi zangu –Zaburi 51:2

**Hadithi ya Krismasi · Luka 2:1-20** | Nitakusifu eh Bwana kwa moyo wangu wote. Nitayasimulia matendo yako yote ya ajabu. –Zaburi 9:1


**Petero Hakua Bila Kasoro · Luka 22:54-62** | Ye yote anayetaka kunifuata ni lazima ajikane nafsi yake, achukue msalaba wake kila siku, anifuate. –Luka 9:23

**Mfariji · Yohana 14:15-31** | Bali mjazwe Roho. –Waefeso 5:18b

**Yesu na Watoto · Matayo 18:1-6** | Tumeuona utukufu wake, utukufu wa Mwanae pekee, aliyetoka kwa Baba aliyejaa neema na ukweli. –Yohana 1:14

**Saulo wa Tarso anakuwa Paulo · Matendo ya Mitume 9:1-22** | Kwa hiyo nendeni mkawafanye watu wa mataifa yote kuwa wanafunzi wangu: mkiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. –Matayo 28:19

**Kipofu Bartimayo · Markoo 10:46-52** | Kwa sababu hiyo Mungu alimuinua juu kabisa na akampa jina ambalo ni kuu kuliko majina yote. –Wafilipi 2:9




# AGANO LA MAOMBI

## Kwa Watoto | Kufundisha watoto jinsi ya kuomba!

**CANDY MARBALLI**

**Na Stephen Eyre**

Kielezo na **Luka Flowers** | Utangulizi na **Jerry Kirk**

**The Prayer Covenant Inc.**
P.O. Box 40841
Cincinnati, OH 45240
**www.theprayercovenant.org**

Hakimiliki@2014 na Candy Marbali.Haki zote zimehifadhiwa.
@2018Agano la maombi ya watoto/michezo uliotolewa na Gamelife77.com. Haki zote zimehifadhiwa.

Haki zote zimehifadhiwa.Hakuna sehemu yeyote inaweza kuchapishwa kwa njia yeyote,kieletroniki,kimekaniki,kunakili nakala,kuskani au njia yeyote ingine bila ruhusa ya mchapishaji kwa kuandikiwa,ila na mhakiki,ambaye anaweza kutaja kifungu kwenye hakiki.Kadi la agano la maombi inaweza kunakiliwa pasipo kubadilishwa.kugeuzwa au kusawazishwa na inapatikana mtandaoni bure kwenye **www.theprayercovenant.org/children**.

Vifaa vya kuongeza agano la maombi la watoto vyapatikana kwenye www.theprayercovenant.org, Na pia matoleo ya bure kwenye lugha kadhaa ya kadi za maombi za agano la maombi,agano la maombi la watoto  kitabu cha ukurasa 24 na agano la maombi kitabu cha kupaka rangi.Kuna punguzo za bei spesheli kwa wanaonunua kwa wingi.

Pasipokuwa na kuelezwa vingine,nukuu za biblia zimetolewa toka BIBILIA TAKATIFU,TOLEO LIPYA LA KIMATAIFA,NIV. hakimiliki 1793,1978,1984,2011 na bibilia ,inc.Imetumika na ruhusa.Haki zote zimehifadhiwa duniani kwote.

Mchoro na Sound press and Granite Creative,inc

ISBN 978-0-9899525-8-3

# Orodha ya yaliyomo


OMBI LA WATOTO ........ 1
UTHIBITISHO ........ 6
KUJITOLEA ........ 8
UTANGULIZI ........ 9
UTAMBULISHI ........ 10
SAMPULI YA SOMO ........ 12

NEEMA ........ 18
UPENDO ........ 26
HURUMA ........ 34
KUTUBU ........ 42
KUABUDU ........ 50
KUJITOLEA ........ 58
KUTEGEMEA ........ 66
KUSHAWISHI ........ 74
UFUASI ........ 82
MAMLAKA ........ 90

TAARIFA LANGU LA AGANO LA MAOMBI ........ 98
UKURASA ZA KUPAKA RANGI ........ 99
UBUNIFU WA ISHARA ZA MIKONO ZA KRISTO ........ 109

# Uthibitisho

*Ni furaha na heshima kubwa kwa biblica-shirika la kitaifa cha bibilia kushirikiana na agano la maombi kwa watoto. Watoto si tu viongozi wa kesho kanisani bali ndio wanaoshiriki Zaidi na wengi zaidi kanisani duniani leo. Maombi ya watoto yana nguvu na shinikizo kwa kuleta watu kwa Kristo duniani kwote. Rasilimali hii itasaidia kukamilisha lengo hili!*

– **LAREAU ANDERSON**, Sr. Mkurugenzi global partneships,Biblica- The International Bible Society

*Sasa ndiyo wakati wakulenga macho yetu kwao, ndio kizazi kipya wanaoleta mabadiliko na wanangoja kuchukua mwanga wa Imani. Agano la maombi la Watoto ndio cheche itumikayo kwa mabadiliko. Kupitia maombi watoto wanainuka na kubadilisha maisha. Agano la Maombi linatumika kama chombo cha kuinua watoto duniani nyakati tumepoteza maadili ya maana yaliyofundishwa na Yesu-Maombi. Agano la Maombi ni wito kutoka kwa Mungu na umefafanuliwa vyema kwenye kitabu cha Candy Marballi .Anatualika kuwakaribisha kizazi kipya cha washirika na waombezi duniani.*

– **LUIS BUSH**, International Facilitator, TWC, Servant, Transform World 2020; Co-Founder 4/14 Movement with Pastor Nam Soo Kim

**Agano la Maombi kwa watoto ni changamoto kwa moyo ya watoto kwenye wito wa kuendeleza ufalme wa Kristo kupitia maombi. Asante Candy kwa kifaa kinacho saidia sana.**

– **GARY L. FROST**, Vice President, Midwest Region and Prayer North American Mission Board

**Agano la Maombi ya watoto ni aina ya ajabu na ya kipekee ya kitabu. Nguvu yake ya kuzingatia, uwazi na kwa undani kirahisi huifanya zawadi kubwa kwa mwili wa Kristo. Naamini Mungu atakitumia kitabu hiki kuinua kizazi wa watoto wenye upendo wa kuzingatia maombi kwenye mizizi ya maneno ya Mungu. kisha kuingia kwenye upako wa kazi ya injili kumtukuza Mungu. Kama baba na kasisi wa maombi nina pendekeza hiki kitabu. Tumfuate Yesu pamoja kwenye sehemu ya maombi pamoja na watoto wetu.**

– **DR. JASON HUBBARD**, Director of Light of the World Prayer Center

*Kitabu hiki kimeonyeshwa na kuandikwa vizuri kama muongozo wa maombi kwa watoto duniani nzima na rasilimali kwa makanisa, mashule na jamii. Kina husisha na pia kueleweka.*

– **ROBERT A. MCDONALD**, Retired Chairman, President and Chief Executive Officer of The Procter & Gamble Company

**Agano la Maombi la Watoto linakushughulisha kirahisi. Kinapatikana kirahisi kwa walimu na vipindi vyake vinajumuisha maombi, maandiko na mazoezi mazuri sana. Inapeana thamani kwa masomo ya shule za Jumapili kanisani kikamilifu kwenye kitabu kizuri Zaidi cha watoto. Napenda Agano la Maombi kwa Watoto kwa sababu inawaingiza watoto kwa nguvu na ushangao wa kuongea na Mungu na kufanya mandiko ya bibilia rahisi na ya kufurahisha. Kitabu kinamkaribisha msomaji kushiriki uzuri wa Mungu maishani mwao huku akipata kusafiri kidijitali hadithi kuu ya agano la Mungu na mwanadamu. Kuna funzo katika kila somo kwa watoto wa rika zote. Kinafurahisha, kinauhodari na ufanisi.**

– **JOSHUA MAHONEY**, Resources Manager - Every Home for Christ

# Uthibitisho

*Siku ya Pentekoste, Mtume Petero alithibitisha uraia kwenye Ufalme wa Mungu na zawadi ya Roho Mtakatifu ni wetu na watoto wetu (Matendo ya mitume 2:39)Agano la Maombi kwa Watoto inaonyesha ukweli wa ahadi ni sawa kwa kanisa la leo na la kale.*

– **SIDNEY MUISYO**, Vice President for Africa Region, Compassion International

*Ni upendeleo mkubwa kushirikiana na Agano la Maombi la Watoto kuomba pamoja ili kila mtu kila mahali apate kumjua Yesu. Maombi ya Watoto yanaleta muungano kwetu wote na yanagusa moyo wa Mungu.*

– **CHERY OSTERLOH**, Global Prayer, Jesus Film Project

*Nina furaha kuuagano na maombi limetengenezwa ili watoto waitumie kwa maisha yao ya sala. Natumaini itakuwa shinikizo kuu kutayarisha watoto duniani kote kuishi maisha ya sala. Kwa hiyo kwa sauti kuu tutangaze, "Njooni watoto mjifunze kuomba na kumuabudu Mungu.*

– **DR. LOU SHIREY**, Director of Clergy Development/Prayer Ministry, International Pentecostal Holiness Church

*Yesu anataka watoto waje kwake. Agano la maombi la watoto inawapa nafasi watoto wa rika zote sio tu kumfuata kindani lakini pia kufurahia kumfuata Yesu na kushirikiana na wenzao.Candy, asante kwa hii rasilimali njema.*

– **DION STEINBORN**, Director's Office of Jesus Film, Project Catalyst

*Kushirikiana na huduma kadhaa, Agano la Maombi la Watoto liko kila mahali likibadilisha maisha. Ninafuraha hii rasilimali itawasha moto zaidi watoto duniani kuungana na mamilioni wengine ambao tayari wanaomba,'Bwana nijaze na Roho Mtakatifu."*

– **GREG STOUGHTON**, Partnership and Project Coordinator, Office of the President for Cru

*Itabadilisha maisha ya watoto kufundishwa umuhimu wa maombi, jinsi ya kuomba na nguvu ya maombi. Kuongezea umuhimu wa maombi, kitabu pia kinawafunza watoto kuhusu upendo wa Mungu kwao na umuhimu wa kutii.*

– **THOMAS E. TRASK**, Former General Superintendent of the Assemblies of God

*Mungu anakuza kizazi kitakacho leta mabadiliko kwa watoto na vijana. Agano la Maombi la Watoto ni Rasilimali njema kufundishwa kuomba sala ambapo Kristo yu katikati maishani mwao na wenzao. Hiyo inapendeza kivipi! Mimi ni mshabiki mkubwa! Napanga kukisambaza kwa marafiki, wafanya kazi wenzangu na hasa wadogo wangu. Nakusihi pia nawe ufanye hivyo.*

– **TOM VICTOR**, President, The Great Commission Coalition, Facilitator, 4 to 14 Window North American Region

Agano la maombi la watoto ni chombo cha kupendeza kibibilia kuunda upendo na ushirikiano wa kindani na mwenyezi Mungu kwa watoto. Nina amini itawashawishi waumini kuomba, kueneza injili na kuwafanya wafuasi watoto kutii zaidi Amri Kuu na Kamisheni kwa upendo mkubwa sana. Asante kwa hiki zawadi cha ajabu kwa mwili wa Kristo!

– **K. MARSHALL WILLIAMS SR.**, Senior Pastor, Nazarene Baptist Church, Philadelphia PA, and President, National African American Fellowship, SBC

# Kujitolea Kwa

**Watoto wote duniani;** *kuueni mkielewa jinsi Baba wa Mbinguni anawapenda sana.*

**Mume wangu mpendwa Vik na watoto wetu,** *Jonathan na Maria, kwa upendo msaada na kunitia moyo.*

**Stephen Eyre, mwandishi mwenzagu,** *kwa neema ya kugawana umaarufu wako, muongozo na kujitolea kwa huu mradi.*

**Jerry Kirk,** *kwa ukarimu na msaada usiopimika kueneza maono ya siku 40 za agano la maombi la watoto wa dunia.*

**Kila mwanamke aliyekuwemo pamoja nasi kutengeneza ombi la Watoto:**
*Amy Kirk, Sharon Mason, Stephanie Plankovitch, Sharon Schatz and Katie Steele.*

**Irma Chon na Katie Stele wa Harakati la 4/14,** *kwa mawazo yenu na muongozo.*

# Utangulizi

Nimeshirikiana na Agano la maombi la watu wazima kwa miaka 45. Ninafurahia kila wakati ninavyoona jinsi Mungu anaipanua na kuikuza huduma hii. Ila Agano la Maombi la watoto ni ajabu kubwa. Sikuifahamu mpaka Candy Marballi alipotushirikisha kwenye maono yake. Candy aliongozwa na Mungu kuunda kamati ya wataalamu wa huduma ya watoto.Candy na wataalamu hao wamejitolea kwa kutoa maisha yao .Walikua na shinikizo la kutoa huduma hii kwa lugha ya watoto. Baada ya kutoa ukurasa ufaao kwa watoto wakatambua umuhimu wake.

Kama cha watu wazima, hiki cha watoto ni chombo cha kuimarisha na kuongoza kwenye sala. Na kama jina lake linavyojitambulisha ni cha watoto. Inawakuta watoto walipo lakini hakitawaacha walivyo. Ni kizuri, kimefupishwa, na kinaurahisi wa kuelewa na kina wapa changamoto ifaao kwa watoto kukua kidini.

Kitabu hiki kimeandikwa hasa kwa Watoto. Lakini nina amini hata wazazi watafaidika--ili waweze kuelekeza watoto wao; na hata walimu wa shule ya kidini ya jumapili kanisani watabarikiwa ili waweze kuwabariki wanafunzi; pia makasisi watabarikiwa na kupata hekima zaidi kubariki elimu ya Kikristo.

Ni kawaida watoto kuomba, ni kawaida watoto kuomba na wazazi wao ambao wanawaamini na kuwapenda. Agano la maombi kwa watoto linawapa wazazi na walimu uwanja wa kukimbia.Ni njia ya maombi ifunguayo watoto kumpenda Mungu na kuwapa amani kila mtoto anayohitaji.

Awali agano la maombi la watoto ilionekana kama muono mzuri. Sasa naona kuitoa ni uamuzi bora zaidi uliofanywa na vingozi wetu. Inaweza kuwa kibiriti kitakacho washa moto wa Agano la Maombi duniani kwote.

**JERRY KIRK**

Founder of The Prayer Covenant

# Utambulishi

## KUFUNDISHA WATOTO JINSI YA KUOMBA

Luka 11 inaanza na wafuasi wakisema “Bwana tufundishe kuomba” Tangu kuchapishwa kwa mara ya kwanza 2014, wakati Tom Victor alitualika kukizindua hiki kitabu katika 4/14 Best practices conference NYC, Mungu ametumia Agano la Maombi la Watoto kueneza injili na kufanya mioyo ya watoto wafuasi wakati wakifundishwa kuomba. Watoto wanaposhiriki nguvu ya maombi kujibiwa, wanafurahia, na imani yao inakua na wanataka kuomba zaidi.

Maombi ni moja yapo kuu ya umuhimu wa nidhamu ya kidini kwa sababu maombi yanakuza uhusiano wetu na Yesu. Tunavyotumia wakati mwingi na Yesu ndivyo tutakua zaidi kama Yesu-tukijazwa na neema, upendo, huruma na kusameheana. Ombi letu ni kitabu hiki kitashinikiza kujitolea kwa maombi kwa watoto na vijana duniani nzima na kukuza kizazi cha wafuasi wanaoelewa maana ya ufuasi wa kweli na upendeleo wa kupata fursa kuwa karibu na Yesu kila siku kwenye sala.

Watoto wanapoonza safari hii, tunataka wapate uzoefu na Mungu njia nyingi za nguvu, kujifundisha kumtii na kuitikia muongozo wa Roho Mtakatifu.

Mungu anaongea na watoto mara tofauti kupitia Roho Mtakatifu. Kujifunza kumskia ni kitu tunatumaini watagundua wanapoanza maisha ya maombi. Colin Milar ni mwaanzishi wa moto wa sala na aliniambia hivi “Mpe Mungu ngoto ya tano” kutoka Zaburi 46:10 inayosema, ‘Tulia na ujue mimi ni Mungu’. Ni mwaliko, kumpa Mungu dakika tano kutulia na kuwa na Mungu mtakatifu zaidi. Wazo nzuri sana kwa watoto na watu wazima. Kwa urahisi alika watoto watumie dakika tano tu kutulia na Mungu kusikiliza anachosema au kuwaelekeza. Tutaeleza zaidi kwenye ukurasa wa kutegemea. Kuskiza Mungu ni muhimu kama kuomba. Anaongea nasi kwa utaratibu kupitia neno lake au Roho Mtakatifu. Samuel mchanga aliweza kuitambua sauti yake na Mungu akamtumia kuingoza taifa.

Utume wetu ni shauku letu: kuongoza watoto na watu wazima kumfuata Yesu kupitia Agano la Maombi. Tunapowapa watoto kifaa hiki, Mungu naye anafanya kazi ndani yao kimuijiza. Tumefikia zaidi ya watoto milioni 2.5 kwenye nchi 53 duniani kwote. Watoto milioni 2.5 wakimfuata Yesu pamoja,wakijifundisha kuisikia sauti yake na kuitii! Naamini huu ni mwanzo tuu.

Hakikisha kuangalia ukurasa wa rasilimali yetu ya Watoto: **theprayercovenant.org/children.** Utakuta rasilimali nyingi, picha na ushuhuda kutoka kwa Agano la Maombi la Watoto kutoka dunia nzima. Tunapenda hadithi! Tafadhali tuandikie na kushiriki nasi hadithi yako ya Agano ya Maombi. Tunangojea kwa hamu kusikia kutoka kwako.

# Utambulishi

## KUJIFUNDISHA KUOMBA

Watoto wako wanaweza kukuuliza, “Agano ni nini?” Kirahisi ni ahadi kati ya watu wawili au zaidi-ahadi ya kuombeana kwa wakati fulani au upendavyo. Watoto wana mahusiani-wazo la kuombeana hata wakiwa wawili au watatu ni rahisi na ya kufurahisha kwao kuelewa. Tunapopitia kila somo hakikihsa kuwauliza, “Mungu anaweza kuwa amekuwekea nani kuweka ahadi ya maombi naye?” au “Njia gani Mungu anaongea nawe kushiriki hadithi yako na wengine?”

Watoto mara nyingi wataanza agano na wazazi, ndugu au marafiki wao. Wanaweza kuingia ahadi mpya wakati wowote. La muhimu ni kuwakuza maisha ya sala. Mara nyingi sana watoto ndio wanaoongoza sala nyumbani kwao.

Tunatumaini unapendela mpangilio, ambao kitabu chote kina sura 10 zinaozingatia: Neema, Upendo, Huruma, Kutubu, Kuabudu, Kujitolea, Kutegemea, Kushawishi, Ufuasi na Uongozo. Kila hadithi ina hadithi ya bibilia, mistari ya kukariri, karatasi ya kazi, aina ya sala fupi, mchezo wa kufurahisha, aina ya wimbo (RAP) na kadhalika. Tafuta hizi alama 10 zinazoshiria kila somo




Mtaala unaweza kubadilishwa. Amua kile kinachokufaa, uwe shule ya jumapili ya kidini, vipindi vya VBS au kikundi kidogo cha wasomaji. Tunapendekeza kikuzindua kwenye awamu mbili. Kwanza wafanye wafuasi watoto kupitia mandhari 10 kwa muda wa wiki 10 kisha uwalike kuweka ahadi na rafiki au jamaa wao. Ukimaaliza mtaala huu, zingatia sala ya muhimu darasani. Kama unavyo tenga muda ya kuabudu kupitia maombi kila wiki ongeza muda wa kuomba na kuabudu. Alika watoto kushiriki:

- Jinsi Mungu anawabadilisha.
- Jinsi Mungu anavyombadilisha wanaye muombea.
- Jinsi Mungu anasema nao.
- Majibu ya maombi
- Nia ya Maombi

Asante kwa ushirikiano wako unaoongoza Watoto kwa Yesu katika nguvu za maombi.



# Neema

## SHUGHULI 1: UNAWEZA KUISEMA??

SHUGHULI 1

### Kukariri Ombi

Baba Mwenyezi Mungu, asante kwa kunipenda na kunifanya mmoja ya watoto wako.

**Soma** ombi lote Pamoja - zingatia kina, kwa mfano, Neema.

**Imba** ombi lote pamoja. *(cheza muziki uliorekodiwa}*

### Kariri maandikio yanayo ambatana (1 Yohana 3:1)

**Shughuli za Fumbo**
Kila neno ni sehemu tofauti ya fumbo. Wanapaswa kuweka kila neno kwa utaratibu kukamilisha aya.

**Shughuli za Ubao Mweupe**
Una kocha aliye andika aya nzima ubaoni. Watoto wanakariri maneno yote pamoja kisha kocha anafuta maneno machache mpaka ayamalize yote na watoto wanapaswa kuyasema kutoka mioyo yao.

**Pangeni Mstari!**
Watoto wapange mstari. Kila mtoto anasema neno lifuatao kwenye aya. wakikosa neno lazima wakae chini(hii ni ngumu kuliko inavyo onekana!)

*Kuwa na zawadi ndogo kwa watakao weza kukariri aya.*

*Watoto washiriki kila aina ya shughuli ya kukariri*

## SHUGHULI 2: UNAWEZA KUIPATA?

Wakati wa mafunzo ya Bibilia - kuchambua kindani neno la Mungu. Kuwa na maandiko yanayo ambatana na kitu fulani. Kuwa na shindano la atakayeweza kuutafuta ukurasa wa Bibilia (aya tatu vifuatazo) haraka zaidi kisha huyo mtu aisome.

Gundua bibilia inasema nini kuhusu NEEMA

**Yohane 3:16**

**1 Yohane 4:10**

**Warumi 8:38-39**

*(Unaweza kutumia aya hizi au zingine)*

**Aya inaniambia nini?**

**Inahusikana na maisha yangu kivipi?**

**Nimejifunza nini kuhusu Neema?**

## SHUGHULI 3: UNAIHISI?

Wakati wa kujadiliana na kushirikiana. Bila-kuhukumiana - watoto wanaweza kusema mashaka yao kuhusu Imani, kuuliza maswali na kusema uwoga wao na kadhalika. Zote hizi zitaleta muono tofauti wa imani. Viongozi wanapaswa kujifungua na kuwaambia hadithi zao kibinafsi juu ya neema maishani mwao. Kuwa wazi na mnyonge na watoto, na watoto pia watafanya hivyo.

Mifano ya maswali ni kama:

**1) Unajuaje Mungu anatupenda?**

**2) Unaonyeshaje mapenzi yako?**

**3) Nini inakufanya kuhisi kupendwa?**

**4) Nini kinatufanya tuwe watoto wa Mungu?**

## SHUGHULI 4: AINA YA MAOMBI FUPI

SHUGHULI 4

Hii ni nafasi ya watoto kuomba pamoja kijumla. Wengine wao wanaweza kuwa hawajawaiomba mbeleni na wanahaya kujaribu. Aina hii ya maombi inafanya kuomba rahisi na ya kufurahisha kwa sababu unapaza sauti neno moja au ombi fupi.Aanza na kufundisha watoto majina ya Mungu na sifa zake. Ni njia ya kumuabudu na kumtukuza Mungu. Watoto wanapenda hivi na kufuatilia haraka sana. Unahisi Roho akipanda kwenye maombi. Kila siku wanakua starehe na wanaweza kushiriki maswala ya maombi ifikapo mwisho wa wiki.

| |
|---|
| **Bwana wa haki** (Yahweh Tsidqenu) |
| **Emmanueli** (Immanue-el) |
| **Baba** (Abba) |
| **Mungu wa milele** (El Olam) |
| **Mungu uliye juu Zaid**i (El Elyon) |
| **Hakimu** (Shophet) |
| **Bwana Mchungaji Wangu** (Yaweh Rohi) |
| **Bwana Mwamba Wangu** (Yahweh Tsuri) |
| **Bwana wa Amani** (Yahweh Shalom) |
| **Mungu Muumba** (Elohim) |
| **Bwana** (Yahweh) |
| **Mungu Anayeniona** (El Roi) |
| **Mungu Mkuu** (El Shaddai) |
| **Mungu Mpaji** (Yahweh Yireh) |
| **Mungu Anayeponya** (Yahweh Rophe) |

Shughuli ingine ya kuomba ni “Kuomba na rangi.” Wekea watoto mziki wa kuabudu kisha waache walale manyasini na kufurahia maumbile ya Mungu muumba - anga, miti na mawingu.Kwenye karatasi kubwa nyeupe waache watoto wachore wanavyohisi kulingana na wanavyoona Mungu akinena nao. Watoto WANAPENDA kuomba na rangi na utaajabika ukiona watakavyo shiriki. Zoezi hili linaweza chukua muda wa dakika 30.

## SHUGHULI 5: IONGEE!

Waache watoto waseme kiwazi maoni yao kuhusu upendo wa Mungu, uoga na fikira zao kuhusu kupoteza upendo wa Mungu au furaha wakifunzwa kuhusu pendo lake kwao.

Mada zingine za kuzumgumzia zinaweza kuwa kama:

Neema inamaanisha kupendwa hata kama hatujafanya lolote kustahili pendo.

Upendo wa milele unamaanishaje? Ni upendo ambao hautaisha! Haitaisha ukifanya kitu kibaya, ukihisi kuogopa. Hautaisha mzazi wako akipoteza kazi. Hautaisha hata kama...... (jaza pengo)

Haijalishi kinakachotokea, Upendo wa Yesu hautaisha na hautawahi kushindwa.

## SHUGHULI 6: UNAWEZA KUISIKIA?

Wakati wa hadithi unapendelewa sana na watoto. Aanza kwa kuwasomea watoto kisha kuuliza maswali. *(dakika 15)*

Chagua watakao jitolea kuwa waingizaji kucheza hadithi ya Bibilia. Mavazi rahisi yatafanya kazi vizuri. Kuwa na kanzu ya mchungaji na mavazi rahisi za nyakati za bibilia kama vitambaa vya kichwa na joho. *(dakika 15)*

Cheza mchezo wa kurudia. Waambie hadithi kirahisi kisha watoto warudie kusema hadithi hiyo. Tengeneza vikundi vya watu nane kisha mtupie mtoto mmoja mpira. Ataanza na mstari mmoja wa hadithi kisha kumtupia mtoto mwengine mpira ambaye atasema mstari ufuatao. Zungusheni mpira kila mtoto akisema mstari mmoja mpaka hadithi yote iishe. *(dakika 15)*

## SHUGHULI 7: UNAWEZA KUFANYA?

UTENDAJI

SHUGHULI 7

Muda wa kujadiliana: jadiliana maswala yafuatayo au tunga yako.

Nawezaje kutumia mafunzo ya leo maishani mwangu?

Nimeonaje neema kwa vitendo?

Nawezaje kuonyesha neema kwa wengine?

## SHUGHULI 8: UCHEZE! (MCHEZAJI MUZIKI kutoka GameLife)

SHUGHULI 8

### Mchezo wa “Mchungaji na Kondoo”

1. LA DHARURA: Huu mchezo unachezwa kama wa ‘Kuiba nyama ya Nguruwe’ una vipande vinne na tofauti kiasi. “kondoo”, “mbwa mwitu” na “mchungaji”
2. Onyesha wachezaji mipaka ya mchezo itakapochezwa-mraba mkubwa. Katikati kuna mraba mdogo ambapo kondoo aliyepotea anaishi. Kuna mbwa mwitu sita wanamlinda kondoo aliyepotea. Wagawanye wachezaji kwenye makundi manne kisha kila kundi likae upande wa nje wa mraba mkubwa
3. Baada ya wachezaji kugawanywa kwa vikundi vinne (vikundi viwili kama una wachezaji chini ya10) kila mchezaji kwenye mstari apewe nambari. Kila kikundi kiwe na nambari mmoja, mbili tatu na kadhalika.
4. Waeleze kocha akisema namba mmoja, wenye nambari hiyo wakimbie na wajaribu kumuokoa kondoo aliye katikati, aliyepotea. Ukishikwa na mbwa mwitu unatolewa hadi raundi ifuatayo.
5. DHARURA. Uwe na “mbwa mwitu” zaidi kuliko “kondoo watakao okolewa”
6. Kondoo HATAWEZA kumuokoa kondoo aliyepotea kwa sababu mbwa mwitu ni wengi zaidi.

7 DHARURA.Cheza tena wakati huu waeleze mmoja wa kocha atakua mchungaji mzuri na anaweza kuwaita wakati wowote. Mbwa mwitu ondokeni! Kondoo nendeni nyumbani! kisha mbwa mwitu watakaa chini na kondoo wataweza kurudi kwa mstari kucheza tena.

- **Ukweli na uhusiano na maisha: Mchungaji Mwema kila wakati anahakikisha kondoo wake wako salama nyumbani.**

## SHUGHULI 9: KAZI YA KARATASI

SHUGHULI 9



Kuwa na nakala za karatasi za kazi. Mmoja ya kila mtoto. Kisha kuwa na kalamu, penseli, penseli za rangi na kreyoni za kufanyia michoro Sio lazima utumie michoro iliyoandikwa bali unaweza kubuni yako swala ni hakikisha kila mandhari.

1. Unaweza kukumbuka mstari wa kwanza wa ombi kisha uliandike hapo chini?
2. Jaza mapengo:

   1 Yohane 3:1, Tazameni ________ (ni pendo) la namna gani aliotupa ________ (Baba) kwamba tuitwe ________ (wana) wa Mungu.
3. Kwa maneno yako mwenyewe tueleze kwanini unadhani wewe ni mtoto wa Mungu milele?
4. Yesu anakufahamu na jina lako. Andika sentensi au chora picha yakuonyesha jinsi jambo hili linakufanya ujihisi.
5. MUDA WAKUJIBU:

   Ni vyema kuwa na shukrani. Hii inampendeza Yesu.Unaweza kumwandikia Yesu ujumbe wa asante? (Unaweza kuwapa watoto penseli za rangi, kalamu kreyoni na vibandiko watumie kutengeneza kadi za asante, ama uchague namna ingine ya ubinifu)

## SHUGHULI 10: NI MUZIKI WA RAP!


SHUGHULI 10




Hii ni moja yapo ya aina zinazopendwa zaidi. Kila mandhari unaisha na RAP. Ina ruhusu watoto kujieleza na ubunifu. Kuwa na vyombo vya muziki kama ngoma, kinanda na vyombo vingine hata vilivyotengenezwa nyumbani. Mchague mtu mmoja kuongoza RAP na wenzake watamjibu vilivyo. Maneno yako kwenye kitabu. Badilisha viongozi. Watoto pia wanaweza kutunga maneno yao yatakayo ambatana na NEEMA.

# Neema

*Baba wa Mbinguni,*
*Asante kwa kunipenda na kunifanya mmoja ya watoto wako.*



**Fumbo la kondoo aliyepotea • Luka 15:1-7**



**1 YOHANA 3:1**

**Tazameni ni pendo la namna gani aliotupa Baba kwamba tuitwe wana wa Mungu.**



# Neema

## UNAWEZA KUIPATA?

*Baba wa Mbinguni, Asante kwa kunipenda na kunifanya mmoja ya watoto wako.*

**1 YOHANA 3:1**

Tazameni ni pendo la namna gani aliotupa Baba kwamba tuitwe wana wa Mungu.

## UNAWEZA KUIPATA?

*Yohana 3:16*

*1 Yohana 4:10*

*Warumi 8:38-39*

## UNAIHISI?

Unajuaje Mungu anatupenda?

Unaonyeshaje mapendo yako?

Nini kinakufanya uwe mtoto wake?

Nini kinakufanya kujihisi kupendwa?

# Neema

## "AINA YA MAOMBI POPCORN" KIPINDI CHA KUJADILIANA

Kama darasa lako ni kubwa, igawe kwa vikundi vidogo na viongoze kwa kusema, ***"Baba wa Mbinguni, asante kwa kunipenda na kunifanya mmoja ya watoto wako."*** Waambie watoto warudie mstari huu kisha uwaambie waombe kwa sentensi moja wakimwambia Mungu wanavyopenda kuwa watoto wake. Jinsi upendo wa milele wa Mungu unamaanisha kwao,na kumshukuru kwa huo upendo. Wanaweza kutaja majina tofauti ya Mungu na sifa zake. Kama darasa lako ni ndogo wanaweza kuunga mviringo kwa kushikana mikono, na kila mtoto atakaye kuomba aendelee.

## IONGEE!

- Neema inamaanishwa kupendwa hata kama hatustahili
- Twafahamu Mungu anatupenda kwa sababu alituumba, anatupatia mahitaji yetu na alimtuma mwanawake wa pekee Yesu kufa msalabani kwa sababu yetu.
- Unafahamu upendo wa milele unamaniisha nini? Inamaana upendo hautawahi isha hata Kwa miaka na miaka
- Hautaisha ukifanya makosa.
- Hautaisha ukiogopa
- Hautaisha mtu umpendaye akifa
- Hautaisha mzazi wako akipoteza kazi
- Hautaisha usipopata alama mzuri shuleni.
- Hata iweje upendo wa Yesu hautawai isha na hautawahi kushindwa.

Wafanye watoto washiriki kiwazi maono yao kuhusu upendo wa Mungu, uwoga wao na pia wasiwasi wao ikiwa watapoteza upendo la Mungu pia furaha yao kujifunza na kusikia kuhusu upendo wa Mungu.

# Neema

## UNAWEZA KUISIKIA?

**Fumbo la Kondoo Aliyepotea (Luka 15:1-7)**

Yesu alitaka kila mtu ajue Mungu anawapenda. Akawapa hadithi kuhusu mchungaji na kondoo aliyepotea. Mchungaji alikuwa na wasiwasi sana kuhusu kondoo aliyepotea hadi akawaacha kondoo wote wengine na kwenda kumtafuta mmoja aliyepotea. Kondoo wakati mwingine wanapotea na kwasababu hawana nguvu simba, umbwa mwitu au dubu wanawashambulia na kuwala. Kazi ya mchungaji nikulinda kondoo wake na hivyo ndivyo alivyofanya. Alipompata alifurahi sana kisha akambeba juu mabegani hadi nyumbani. Kisha akaita marafiki wake na majirani kusherehekea kondoo mmoja aliyepotea kupatikana. Yesu akasema hivi ndivyo itakuwa mbinguni mvulana mmoja, au msichana, Mwanaume au mwanamke akikubali kumpokea kama Mwokozi wake. Wanapotoka kupotea hadi kupatikana na hii inaleta furaha kubwa na kusherekea mbinguni! Zefania 3:17 tusaidie kuhisi raha ya Baba yetu wa mbinguni anayo kwa watoto wake. “Mungu mwenye Nguvu atatuokoa. Atatufurahia na kututuliza na upendo wake, atatufurahia kwa kuimba.” Hiyo inakufanya ujihisi vipi?



## UNAWEZA KUFANYA?

- Amini Yesu alikufa kwasababu ya dhambi zako na anaishi moyoni mwako.
- Amini neema yake imekufanya mtoto wake mpendwa
- Amini upendo wake hautawai isha hata iweje.
- Amini Mungu anaweza kukutumia kueneza injili yake ya neema kwa mtu leo.

# Neema

## UCHEZE!

### Mchezo wa “Mchungaji na Kondoo”

1. LA DHARURA: Huu mchezo unachezwa kama wa ‘Kuiba nyama ya Nguruwe’ una vipande vinne na tofauti kiasi. “kondoo”, “mbwa mwitu” na “mchungaji”
2. Onyesha wachezaji mipaka ya mchezo itakapochezwa-mraba mkubwa. Katikati kuna mraba mdogo ambaopo kondoo aliyepotea anaishi. Kuna mbwa mwitu sita wanamlinda kondoo aliyepotea. Wagawanye wachezaji kwenye makundi manne kisha kila kundi likae upande wa nje wa mraba mkubwa
3. Baada ya wachezaji kugawanywa kwa vikundi vinne (vikundi viwili kama una wachezaji chini ya10) kila mchezaji kwenye mstari apewe nambari. Kila kikundi kiwe na nambari mmoja, mbili tatu na kadhalika.
4. Waeleze kocha akisema namba mmoja, wenye nambari hiyo wakimbie na wajaribu kumuokoa kondoo aliye katikati, aliyepotea. Ukishikwa na mbwa mwitu unatolewa hadi raundi ifuatayo.
5. DHARURA. Uwe na “mbwa mwitu” zaidi kuliko “kondoo watakaoo okolewa”
6. Kondoo HATAWEZA kumuokoa kondoo aliyepotea kwa sababu mbwa mwitu ni wengi zaidi.

7 DHARURA.Cheza tena wakati huu waeleze moja wa kocha atakua mchungaji mzuri na anaweza kuwaita wakati wowote. Mbwa mwitu ondokeni! Kondoo nenedeni nyumbani! Kisha mbwa mwitu watakaa chini na kondoo wataweza kurudi kwa mstari kucheza tena.

- **Ukweli na uhusiano na maisha: Mchungaji Mwema kila wakati anahakikisha kondoo wake wako salama nyumbani.**

## MASWALI

1. Kwenye raundi yakwanza wa mchezo kuna mtu aliweza kuwaokoa kondoo kutoka mbwa mwitu? (La) Kwanini?
2. Kwenye Bibilia mchungaji aliendа kuokoa kondoo wangapi? Mmoja tu! Wavulana na wasichana unafahamu kama wewe ungekuwa kondoo aliyepotea mchungaji mwema Yesu angekuja kukutafuta? Unahisi vipi ukifahamu kuwa kila wakati Yesu anakutafuta?
3. *Tuombe.Rudia baada yangu. Asante Mungu tumefurahia mchezo huu, nifundishe kuelewa neema ni kitu napokea bila kuifanyia kazi. Ni zawadi.Tutulie na kuskiza Mungu anaposema nasi. Nimeulizia hii zawadi ya Neema? (**tulia) Mungu asante kunifanya mmoja ya watoto wako. Mimi ni mtoto wa Mungu!

**{Viongozi haya maombi ni ya ‘rudia baada yangu’ wavulana na wasichana rudia baada yangu….}*
***{viongozi tulia kwa sekunde 10 mkimruhusu Mungu kusema na moyo wa kila mtoto.*
*Tunawafunza watoto kuongea katika maombi na pia kusikiliza}*

©2018 cha Agano la Maombi Kwa Watoto / Michezo iliyotolewa na GameLife77.com. Haki zote zimehifadhiwa.



# Neema

## KAZI YA KARATASI

❶ **Unaweza kukumbuka mstari wa kwanza wa ombi kisha uliandike hapo chini?**

❷ **Jaza mapengo.**

**I Yohana 3:1: Tazameni _________ la namna gani aliotupa _________**

**kwamba tuitwe _________ wa Mungu.**

❸ **Kwa maneno yako mwenyewe tueleze kwanini unadhani wewe ni mtoto wa Mungu milele?**

❹ **Yesu anakufahamu na jina lako. Andika sentensi au chora picha yakuonyesha jinsi jambo hili linakufanya ujihisi.**

❺ **MUDA WAKUJIBU:**

**Ni vyema kuwa na shukrani. Hii inampendeza Yesu.Unaweza kumwandikia Yesu ujumbe wa asante? (Unaweza kuwapa watoto penseli za rangi, kalamu kreyoni na vibandiko watumie kutengeneza kadi za asante, ama uchague namna ingine ya ubinifu)**

# Neema

## NI WIMBO WA 


**Mimi ni mtoto mpendwa wa Mfalme wa wafalme!**

**NI MIMI, NI MIMI!**

**Mimi ni kiumbe chake cha thamani milele!**

**NI MIMI, NI MIMI!**

**Nimeokolewa na neema yake na kukombolewa na damu yake!**

**NI MIMI, NI MIMI!**

**Nimefunikwa na manyoa yake na salama toka madhara!**

**NI MIMI, NI MIMI!**

**Nashukuru kwa upendo wake ambao hutawaisha!**

**NI MIMI, NI MIMI!**

**Mimi ni mtoto wa Mungu mkuu Zaidi!**

**Amina!**

Mwalimu anaongoza kwa kusoma maneno ya rangi nyeusi kisha watoto watamjibu na maneno ya rangi ya samawati.Baadae wahimize darasa waandike muziki wa rap kama kikundi,wakiandika fikira zao kwenye ubao. Waangalie watakavyo kuwa na furaha wanapo imba walichoandika.

# Upendo

***Nisaidie kukupenda na kukutii.***



**Hadithi ya Abrahamu • Mwanzo 12:1-5**



**MATHAYO 22:37,38**

**Mpende Bwana Mungu wako na roho yako yote na moyo wako wote na akili yako yote. Hii ndiyo amri ya kwanza na kuu zaidi.**



# Upendo

## UNAWEZA KUIPATA?

*Nisaidie kukupenda na kukutii.*

**MATHAYO 22:37-38**

Mpende Bwana Mungu wako na roho yako yote na moyo wako wote na akili yako yote. Hii ndiyo amri ya kwanza na kuu zaidi.

## UNAWEZA KUIPATA?

*Kumbukumbu 7:9*

*Yohana 14:15*

*2 Yohana 1:6*

*Wakolosai3:20*

## UNAIHISI?

Kutii ni nini?

Upendo una muhimu zaidi ya kutii?

Upendo unahusikaje na kutii?

# Upendo

## “AINA YA MAOMBI POPCORN” KIPINDI CHA KUJADILIANA

Waongoze watoto wakati wao wa maombi kusema, ***“Nifundishe kukupenda na kukutii.”*** Wafanye watoto warudie ombi. Washawishi kuomba maombi ya sentensi moja wakimwomba Mungu jinsi kujifunza kumpenda na kumtii. Wanaweza kutumia majina ya Mungu tofauti na sifa zake ilioshirikiwa katika Somo la Mfano.

## IONGEE!

- Yesu anataka tuwaheshimu wazazi wetu
- Yesu anataka tumtii. Hii inamfuraisha.
- Tunamuonyesha Mungu mapenzi yetu tukimtii kwa vitu vyote.
- Utaona kwa hadithi kuwa kutii unafwatwa na Baraka.
- Kumheshimu na kumfwata Yesu ni safari ya kufurahisha.

Hapa unaweza kuanza kuongea juu ya heshima. Tukiwaheshimu wazazi wetu tunamtii Mungu, kwa maana alisema tunapaswa kuwatii wazazi wetu kwa vitu vyote. Waache watoto waeleze ugumu wanaopata kutii na wanavyo faidika wanapokuwa na heshima. Kisha, wasaidie kuona jinsi upendo na kutii vinaambatana.

# Upendo

## UNAWEZA KUISIKIA?

**Hadithi ya Abrahamu (Mwanzo 12:1-5)**

Abraham aliishi miaka mingi iliyopita. Alipokuwa mzee sana, Mungu alimwambia, "Ondoka nchi yako na jamii na ndugu zako kisha utaenda kwa nchi ntakayo kuonyesha. Ntakubariki na kufanya kizazi chako taifa kuu. Utatambulika na kuwa baraka kwa wengine." Kila mtu duniani atabarikiwa kwa sababu yako. Abrahamu akamtii Mungu. Akaondoka na mke wake Sara, mpwa wake Lot na vitu vyao vyote. Wakaenda mbali sana na nyumbani kwao, kutoka mji uitwao Heron hadi nyumbani kwao mpya walioita nchi ya ahadi. Unawaza kwanini Abrahamu alifanya alivyo ambiwa na Mungu? Ndiyo umepata! alikuwa anajifundisha kupenda na kutii. Kutii kwake ulikuwa tu mwanzo wa maisha yake ya kutii, kupenda na kuamini.



## UNAWEZA KUFANYA?

- Muonyeshe Mungu mapenzi yako na kujitolea kwa kutii anachosema.
- Waheshimu wazazi wako kwasababu hii inamtukuza Mungu
- Jitolee kumpenda Mungu na moyo ,roho, akili na nguvu yako yote.

# Upendo

## UCHEZE!

### Usiangalie nyuma

1. Wagawe wachezaji kwenye vikundi vya wachezaji 10. Kila kikundi wanashikana mikono na kufanya mviringo. Weka mikono na uso wako chini nyuma ya yule mtu aliye kulia kwako ukimtazama "mkia".
2. Peana mikia mitatu {kipande cha nguo au Kamba ambacho kitavutika kirahisi} kwa wachezaji wote na wavitie kwenye suruali zao, sketi au kwenye mikanda ikiwezekana. [ Kwa wachezaji watakayo kosa kwa kuweka mkia,wafunge kipande cha nguo kiunoni kisha uweke mkia hapo] {kama mika haitapatikana utamgusa tu mchezaji aliye mbele yako]
3. Waeleze chanzo cha mchezo huu ni wachezaji kuvuta mkia wa mchezaji aliye mbele yake. Mkia wako ukitolewa unatoka mchezoni raundi hii.
4. DHARURA: Waeleze kwa mchezo kufanikishwa, wachezaji wasiangalie nyuma lakini washughulike na waliombele zao-lengo lao.
5. DHARURA: Kama kukimbizana kwenye mviringo (ukijaribu kufikia mkia mbele yako) ni ngumu (ni vigumu kama wachezaji ni wachache) chezeni kwenye mraba mkubwa.Sema anza kisha wachezaji wajaribu kulinda mikia yao huku wakijaribu kutoa ya wachezaji wengine.
6. Kocha akisema 'simameni' wachezaji waliosalia na mikia yao ndiyo washindi.

- **Ukweli na Uhusiano na Maisha: Abrahamu aliitwa na Mungu kwenda nyumbani kwengine. Abrahamu aliwacha vitu vyote alivyozoea, nyumba yake, wazazi wake, kazi yake. Kuangalia mbele, Abrahamu alimtii Mungu na Mungu mwenyezi alimbariki sana.**

## MASWALI

1. Huyo mchezo ulikuwa wa kufurahisha! Ni ya maana kuangalia mbele-je ingeakuaje mchezaji angegeuka nyuma kuangalia mkia wake ?(mchezaji angeenda polepole na kupoteza mkia wake)
2. kwenye bibilia ni vitu gani Abrahamu aliviacha kuenda mbele na kumfuata Mungu? ( Ardhi yake,kazi yake,na marafiki)
3. Yesu asante kunita hapa leo. Nionyeshe jinsi ya kukutii na kukupenda na moyo wangu wote, roho na akili yote .( tulia) Mungu nakupenda,nataka Yesu anisaidie kukutii.

©2018 cha Agano la Maombi Kwa Watoto / Michezo iliyotolewa na GameLife77.com. Haki zote zimehifadhiwa.



# Upendo

## KAZI YA KARATASI

1. Unaweza kumbuka mstari wa pili wa maombi, UPENDO, kisha uiandike hapo chini?

2. Jaza mapengo.

   Mathayo 22:37-38: ____________ Mungu na ____________ wako

   yote ____________ ____________ . Hii ndiyo ____________ kuu

   na ____________ .

3. Inamaanisha nini kutii?

4. Unafikiria kitu gani ni kigumu zaidi kuhusu kutii?

5. MUDA WAKUJIBU:

   Kwenye karatasi ya mistari tumia uandishi wako bora zaidi kuandika aya ya kukariri ya leo kisha ibandike kwa karatasi ya rangi uipendayo – karatasi hii ya rangi inapaswa kuwa kubwa ili iwe kama fremu. Unaweza kuibandika kwenye ukuta wa chumba chako cha kulalia au kwenye dawati lako kukumbusha juu ya amri kuu zaidi ya Mungu.

# Utiifu

## NI WIMBO WA




**Ufanye nini mwanzo wa kila siku?**

**AMINI, TII NA OMBA!**

**Ufanye nini ukisoma Neno Takatifu la Mungu?**

**AMINI, TII NA OMBA!**

**Ufanye nini ukishawishika kufanya dhambi?**

**AMINI, TII NA OMBA!**

**Ufanye nini ukiwa na siku mbaya Zaidi?**

**AMINI, TII NA OMBA!**

**Ufanye nini ukiogopa usiku?**

**AMINI, TII NA OMBA!**

**Ufanye nini kitakacho mpendeza Mungu machoni mwake?**

**AMINI, TII NA OMBA!**

Mwalimu anaongoza kwa kusoma maneno ya rangi nyeusi kisha watoto watamjibu na maneno ya rangi ya samawati.Baadae wahimize darasa waandike muziki wa rap kama kikundi,wakiandika fikira zao kwenye ubao. Waangalie watakavyo kuwa na furaha wanapo imba walichoandika.

# Huruma

*Nisaaidie kupenda*
*wengine unavyonipenda.*



**Msamaria Mwema • Luka 10:25-37**



**YOHANA 15:12**

**Amri yangu ni hii, pendaneni kama nilivyowapenda.**



# Huruma

## UNAWEZA KUIPATA?

*Nisaaidie kupenda wengine unavyonipenda.*

**YOHANA 15:12**
Amri yangu ni hii, pendaneni kama nilivyowapenda.

## UNAWEZA KUIPATA?

*Mathayo 5:44-48*

*1 Wakorintho 13:4-7*

*1 Yohana 4:7-11*

*1 Yohana 3:18*

## UNAIHISI?

Ni nani tunayeamrishwa kumpenda?

Tunafaa kupenda aje?

Ni wakati mgani tunayehisi upendo wa familia yetu?

Wakati mgani tunahisi upendo wa Mungu?

# Huruma

## "AINA YA MAOMBI POPCORN" KIPINDI CHA KUJADILIANA

Waongoze watoto kwenye sala wakiomba hivi, ***"Nifunze kuwapenda wenzangu kama unavyonipenda."*** waambie watoto warudie ombi hili. Washawishi waombe maombi ya sentensi moja wakimuomba Mungu kuwaonyesha jinsi ya kupenda wengine. Wanaweza kumwita Mungu kwa majina yake ya sifa.

## IONGEE!

- Kupenda wenzetu ni la muhimu na sawa na kumpenda Mungu, na moyo wako na roho yako na akili yako yote.
- Kupenda wenzako inamaanisha kupenda rafiki na hata adui zako. Lo! Hilo ni gumu.
- Kupenda wenzetu iwe kwa kujitolea kama Yesu alivyofanya. kumaanisha uweke wengine kabla yako.

Washawishi watoto kuongea kiwazi kuhusu wasiwasi na changamoto kupenda wenzao jinsi Yesu anavyotaka. Tafakari aya kwenye Mathayo 5 watoto wanaweza kutaka kuongea kuhusu changamoto kwenye mahusiano na jinsi ni vigumu kupenda wale ambao hawawapendi. Ongea kuhusu aina ya mapendo kama ilivyo andikwa kwenye 1wakoritho 13. Zipi ni ngumu na zipi ni rahisi kufuata.

# Huruma

## UNAWEZA KUISIKIA?

**Msamaria Mwema (Luka 10:25-37)**

Inaamanisha nini kumpenda mwenzangu kama Yesu anavyotupenda? Tufahamishane. Mtu alimuuliza Yesu, "Jirani yangu ni nani?" Yesu akaeleza kwa hadithi. Alifanya hivyo mara nyingi. Yesu alipenda kupeana hadithi. Akasema. "Mwanaume mmoja alikuwa barabarani akitoka Yerusalemu akielekea Jeriko kisha akashambuliwa na gengi la wanaume wabaya, wakamwibia pesa zake na kila kitu alichokuanacho, wakamuacha nusu mfu kando ya barabara. Kasisi akapita na alipomuona akavuka upande mwingine wa barabara." Kati yangu na wewe huyo mtu hakuwa na huruma. Yesu akaendelea, "Mlawi, kiongozi wa dini pia akapita kando ya huyu mtu, yeye pia akavuka barabara. Jamani, unajua kilichotendeka? Msamaria (waliodharauliwa na wayahudi) alimuona mtu aliyejeruhiwa, unajua alifanya nini? Alionyesha mapenzi ya Mungu kwa kumsaidia na kumtunza. Alimsafisha vidonda kisha akamfunga bandeji, akamuweka kwenye punda wake na kumpeleka hotelini. Akamwambia mwenye hoteli amwangalie hadi atakapo pona. Msamaria akampa mwenye hoteli sarafu za fedha kulipia garama zote kisha akamuambia ikiwa garama zitaongezeka nikirudi nitakulipa". Unajua Yesu alivyoimaliza hadithi? "Enendeni mkafanye hivyo hivyo."



## UNAWEZA KUFANYA?

- Kupenda kwa kujitolea kama Yesu.
- Kupenda kwa vitendo sio tu maneno. Ukiwajali wengine unaonyesha huruma.
- Mpende Yesu na moyo wako wote na muulize Roho Mtakatifu akusaidie kupenda wengine.

# Huruma

## UCHEZE!

### Kikombe kisichoisha

1. Wagawanye wechezaji kwenye vikundi viwili (zaidi kama una watoto wengi)
2. Wasimamishe wachezaji kwenye mstari bega kwa bega lakini waachane kwa mkono ukinyoshwa
3. Mbele ya kila mstari weka ndoo kubwa na pia kwenye mwisho wa mstari.
4. Mpe kila mchezaji kikombe kidogo cha karatasi.
5. Unapowambia "anzeni" mchezaji wa kwanza anaenda kwenye ndoo ya mbele anachota maji, anakimbia arudi kwenye mstari na kumtilia mchezaji amfuataye hayo maji kwa kikombe chake-sio kuyaweka maji bali kumtilia mchezaji amfuataye hadi wamfikie wa mwisho. Huyu wa mwisho anayamwaga maji kwenye ndoo iliyo nyuma ya mstari kisha kuitana, "Nisaidie, nahitaji maji zaidi."
6. Mchezaji wa kwanza akisikia hivyo, anakimbia kwenye ndoo ya mbele achote maji kwenye kikombe chake kisha kupitishia mchezaji anaye mfuata na wanafanya hivyo wakirudia.
7. KWA DHARURA KWA MAKOCHA: Kwenye raundi ya kwanza tia maji kidogo kwenye ndoo, raundi zifuatazo ongeza maji zaidi kwenye ndoo ya mbele ili watoto wapate maji mengi zaidi ya kupitishiana.
8. SABABISHO YA FURAHA: Weka alama katikati ya ndoo ya mwisho na uwambie watoto lazima wapite alama hiyo chini ya dakika tano.

- **Ukweli na Uhusiano na Maisha: Tutapea wengine tulichopokea kutoka kwa Mungu.**

## MASWALI

1. Wavulana na wasichana mbona mliendelea kupeana maji kwa mwenzako? Mbona hukuyaweka maji? (nilivyopeana maji ndivyo nilipata maji Zaidi)
2. Kwenye bibilia kuna mtu aliyekua ameumia na alitaka usaidizi. Unadhani kwanini Msamaria Mwema alikuwa mkarimu kwa mtu aliyeumia na kumsaidia? (huyu mtu alikuwa na hitaji na msamaria aliwezakutimiza mahitaji)
3. Mungu yaweke macho yangu wazi niweze kuona wanao hitaji usaidizi wangu na pia wanaohitaji huruma. Yesu tafadhali nionyeshe hivi sasa anayehitaji msaada wangu. (tulia) Yesu nisaidie kupenda wenzangu na kuwa msaidizi.

©2018 cha Agano la Maombi Kwa Watoto / Michezo iliyotolewa na GameLife77.com. Haki zote zimehifadhiwa.



# Huruma

## KAZI YA KARATASI

1. Unakumbuka mstari wa tatu wa maombi, HURUMA na uiandike hapo chini?

2. Jaza mapengo.

   Yohana 15:12: ___________ yangu ni ___________ mwenzako

   kama vile ___________ wewe.

3. Mbona kifo cha Yesu msalabani ni mfano mwema ya mapenzi yake kwako?

4. Taja njia moja unaonyesha mapenzi ya kujitolea kwa mtu unamjua.

5. MUDA WAKUJIBU:

   Ukitumia karatasi ya kuchoroa na kreyoni na kalamu za rangi nzito,mtengeneze kadi mtu unataka kumuonyesha upendo. Unaweza kumwandikia aya ya kukariri ya leo kwenye hiyo kadi.

# Huruma

## NI WIMBO WA




**Nakupenda Mungu na moyo wangu yote!**

**NDIYO, NDIYO!**

**Nakupenda Mungu na roho yangu yote!**

**NDIYO, NDIYO!**

**Nakupenda Mungu na akili yangu yote!**

**NDIYO, NDIYO!**

**Nakupenda Mungu na nguvu yangu yote!**

**NDIYO, NDIYO!**

**Pendo lako nikitu nataka kuona nakuhisi!**

**NDIYO, NDIYO!**


**Nataka kuwaonyesha wenzangu pendo lako ni la kweli!**

**NDIYO, NDIYO!**

Mwalimu anaongoza kwa kusoma maneno ya rangi nyeusi kisha watoto watamjibu na maneno ya rangi ya samawati.Baadae wahimize darasa waandike muziki wa rap kama kikundi,wakiandika fikira zao kwenye ubao. Waangalie watakavyo kuwa na furaha wanapo imba walichoandika.

# Kutubu

*Najuta dhambi zangu. Nitakase.*



Fumbo la Mfanyakazi Asiyesamehea • Mathayo 18:21-35



**ZABURI 51:2**

**Nioshe kabisa hatia yangu na unitakase dhambi zangu.**



# Kutubu

## UNAWEZA KUIPATA?

*Najuta dhambi zangu. Nitakase.*

**ZABURI 51:2**
Nioshe kabisa hatia yangu na unitakase dhambi zangu.

## UNAWEZA KUIPATA?

*Mathayo 6:9-15*

*Matendo 3:19*

*1 Yohana 1:9*

## UNAIHISI?

Unasikiaje ukifanya kitu cha makosa?

Unasikiaje ukisamehewa?

Nini kinaweza kukuzuia kusema naomba msamaha?

# Kutubu

## "AINA YA MAOMBI POPCORN" KIPINDI CHA KUJADILIANA

Waongoze watoto kwenye sala wakiomba hivi, ***"Naomba msamaha kwa dhambi zangu. Nitakase."*** waambie watoto warudie ombi hili. Washawishi waombe maombi ya sentensi moja wakimuomba Mungu na maneno yao awasamehe na/ama kuwasaidia kuwasamehe wengine. Wanaweza kumwita Mungu kwa majina yake ya sifa.

## IONGEE!

- Ni nini kigumu sana kwako kuelewa kuhusu msamaha?
- Kwanini inaweza kuwa vigumu kusamehe waliokuumiza?
- Kwanini ni vigumu kusema, "pole, naomba unisamehe?"
- Unahisi vipi baada ya kusema ukweli mbele ya Mungu, wazazi wako, ndugu zako au marafiki?

Ongoza mjadala kuhusu utayari wa Mungu kusamehea dhambi zetu zote. Yeye ni mfano wetu na kwa sababu anatusamehea tunapaswa kuwa tayari kuwasamehe wengine. Munaweza kusoma sala ya Baba yetu pamoja. Washawishi watoto kuongea na uhuru juu ya wakati walipoona ugumu wa kusamehea, na walinganishe na wanavyosikia wakisamehewa.

# Kutubu

## UNAWEZA KUISIKIA?

**Fumbo kuhusu Mfanyakazi Asiyesamehea (Mathayo 18:21-35)**

Petero alimuuliza Yesu.'Unapaswa kumsamehea mara ngapi mtu anayekukosea, mara saba?'Yesu akamjibu "sabini mara saba" kisha akawapa hadithi. Kulikuwa na mfalme aliyewaita wafanyakazi wake wamwambie anayemdai. Moja yapo ya wafanyakazi alimdai mfalme pesa nyingi na hangeweza kumlipa. Mfalme akasema, 'Nitakuuza na jamii yako kama watumwa ilinipate pesa zangu ninazowadai." Mfanyakazi akalia, 'tafadhali usifanye hivyo. Tuonyeshe mimi na jamii yangu huruma.' Mfalme alikuwa mtu mkarimu na aliwaonea huruma akawaambia 'nawapa uhuru na kuwasamehea deni' lakini la kushangaza mfanyakazi huyo alifanya nini? Alienda akamtafuta mfanyakazi mwenzake aliyekua na deni lake. Kisha akamwambia usiponilipa kila senti nazokudai nitakutupa gerezani. Mwenzake akaomba, 'tafadhali nipe muda, naomba hurumua.' Lakini mfanyakazi hakuwa na huruma alikuwa na roho ya ukatili. Kisha akampeleka jela. Haikua muda mrefu kabla mfalme alipopata habari hizo. Akakasirika sana akasema, 'wewe mfanyakazi mkatili 'Nilikusamehea deni kubwa kwa sababu uliniomba. Kwanini hukumuonyesha mwenzako huruma? Unajua mfalme alifanyaje? Akamtia gerezani hadi deni lake lote lilipwe.



## UNAWEZA KUFANYA?

- Tubu dhambi zako kila siku ukimuomba Mungu akutakase uwe mweupe kama theluji.
- Amini Mungu anaosha dhambi zako.
- Muombe Mungu akusaidie usitende dhambi.
- Muombe Mungu akusaidie uwe mtu wa kusamehea na ukarimu.
- Uwe tayari wakati wote kusamehea wengine bila kuwa na kisasi dhidi yao.

# Kutubu

## UCHEZE!

### Taa nyekundu taa ya manjano

1. Waonyeshe wachezaji watakapo anzia na kumalizia mchezo.
2. Waongoze wachezaji kusimama kwa mstari nyuma ya mstari wa kuanzia
3. Waeleze kiongozi akisema taa ya manjano wachezaji wanakimbia kuelekea mstari wa kumaliza. kiongozi akisema taa nyekundu wachezaji wanapaswa kusimama mara moja. Wachezaji ambao hawatasimama wakiambiwa taa nyekundu wanarudi hadi mstari wa kuanzia.
4. Kocha atasimama kwenye mstari wa kumalizia na awape mgongo wachezaji. Atabadilisha kusema taa ya manjano na taa nyekundu. Mchezaji atakayemfikia kiongozi alipo ndiye mshindi.
5. Kocha akisema taa nyekundu anapenduka kuhakikisha wamesimama. Mchezaji ambaye bado anakimbia baada ya kocha kusema taa nyekundu amevunja sharia na lazima asimame, arudi mstari wa kuanzia na aanze tena.
6. Chezeni raundi kadhaa.

- **Ukweli na Uhusiano na maisha: Huu ni mfano wa kutubu. Mtu akivunja sharia ni lazima asimame, ageuke na arudi hadi mwanzo na kuanza tena.**

## MASWALI

1. Kwenye mchezo ulipaswa kufanya nini kama kiongozi amesema taa nyekundu na bado unakimbia au kuanguka? (Utasimama, ugeuke, urudi nyuma kisha uanze tena)
2. Kwenye bibilia mfanyakazi alipata neema na msamaha kutoka mfalme? (ndiyo) kisha mfanyakazi huyo alimuonyesha mwenzake neema na huruma kwa aliyemdai pesa? (hapana) Mfalme alipendezwa au kuchukia mfanyakazi alichofanya? (alichukizwa)
3. Yesu unatupa msamaha na neema. Nikifanya vitu sitakikani kufanya nikumbushe kutubu, kusimama, kugeuka, kujirudia na kurudi mwanzoni. Nionyeshe sehemu ambazo napaswa kukiri (tulia) Asante kwa neema, kwa kuniosha, kunitakasa na kunisamehea Bwana Mungu. Niwasamehe wengine pia.

©2018 cha Agano la Maombi Kwa Watoto / Michezo iliyotolewa na GameLife77.com. Haki zote zimehifadhiwa.



# Kutubu

## KAZI YA KARATASI

1. **Unakumbuka mstari wa 4 wa maombi, KUTUBU.**

2. **Jaza mapengo.**

   **Zaburi 51:2: Nioshe na _____________ wangu wote**

   **unitakase _____________ zangu.**

3. **Kwanini tutubu dhambi zetu kwa Mungu kila siku?**

4. **Kwanini inamaana tuwasamehe wenzetu?**

5. **MUDA WAKUJIBU:**

   **Viungo vya Msamaha: Kata vipande vya karatasi kisawa. upande mmoja wa karatasi andika “Mungu ananisamehea niki…” nyuma yake andika “ninawasamehea wengine wakati…” Kisha vianike chumbani kwako kama ukumbusho kumshukuru Mungu kwa msamaha wake usioisha.**

# Kutubu

## NI WIMBO WA RAP!

**Tufanya nini tukikosa kutii?**

**TUBU, OMBA NA GEUKA!**

**tufanye nini tukisema kitu kwa makosa?**

**TUBU, OMBA NA GEUKA!**

**Tufanye nini tukisema uongo?**

**TUBU, OMBA NA GEUKA!**

**Tufanye nini tukianzisha vita?**

**TUBU, OMBA NA GEUKA!**

**Tufanya nini tusipo samehea?**

**TUBU, OMBA NA GEUKA!**

**Tufanye nini tukiwa wakatili?**

**TUBU, OMBA NA GEUKA!**

**Tufanye nini tukitaka vitu kivyetu?**

**TUBU, OMBA NA GEUKA!**

Mwalimu anaongoza kwa kusoma maneno ya rangi nyeusi kisha watoto watamjibu na maneno ya rangi ya samawati.Baadae wahimize darasa waandike muziki wa rap kama kikundi,wakiandika fikira zao kwenye ubao. Waangalie watakavyo kuwa na furaha wanapo imba walichoandika.

# Kuabudu

*Nitakusifu na moyo wangu wote!*





**ZABURI 9:1**

**Nitakusifu eh Bwana na moyo wangu wote. Nitaitangaza sifa yako njema.**



# Kuabudu

## UNAWEZA KUIPATA?

*Nitakusifu na moyo wangu wote!*

**ZABURI 9:1**
Nitakusifu eh Bwana na moyo wangu wote. Nitaitangaza sifa yako njema.

## UNAWEZA KUIPATA?

*Zaburi 145*

*Mathayo 21:16-17*

*1 Wathesalonike 5:18*

*Ufunuo 4:8-11*

## UNAIHISI?

Sifa ni nini?

Ninawezaje msifu Mungu?

Ni wakati mgani naweza kumsifu Mungu?

# Kuabudu

## "AINA YA MAOMBI POPCORN" KIPINDI CHA KUJADILIANA

Ongoza watoto kwa maombi wakisema, ***"Nitakusifu eh Bwana na moyo wangu wote."*** Washawishi watoto warudie ombi. Wahimize kuomba sentensi moja ya kusifu na kuabudu-wakimwambia Mungu jinsi yeye ni mkuu, mzuri na mwema. Inaweza kuwa mstari wa nyimbo ya kuabudu ikiongea kuhusu ukuu wa Mungu au chochote wanataka kumwambia Mungu. Wanaweza kutaja majina tofauti ya Mungu au sifa zake.

## IONGEE!

- Wakati mwingine ni rahisi kuliko wengine kumsifu Mungu.
- Shiriki wakati unahisi ni rahisi kumsifu Mungu.
- Shiriki wakati unahisi ni ngumu zaidi kumsifu Mungu.
- Kuwa na moyo wa shukrani sio tuu  kumpendeza Mungu bali ni sehemu ya kumsifu. Msifu ukiamka! Msifu wakati unakula! Msifu ukienda shule nakurudi! Msifu kabla ya kulala!
- Kukuza tabia ya kusifu hakutampendeza tu Baba yako wa mbinguni bali itakufanya ujisikie mwenye furaha na kubarikiwa!

Watoto wanajua kuabudu! Hawajizui kuonyesha upendo wao kwa Yesu, inaweza kusambaa kwa wenzao. Wacha washiriki mtindo gani wa kuabudu wanaopenda zaidi. Hakikisha kuzungumza juu ya shukrani. Ni vigumu kushukuru kwa ajili ya kila kitu kila wakati. Hakuna wakati unaweza kuwa umechelewa sana kukuza tabia ya sifa na shukrani.

# Kuabudu

## UNAWEZA KUISIKIA?

**Hadithi ya krismami (Luka 2:1-20)**

Zamani za kale zaidi ya miaka elfu mbili iliyopita, Binti aitwae Maria alitembelewa na malaika Gabriel. Alikuwa na ujumbe maalum wake. ‘Usiogope Maria. Unaoupendeleo wa Mungu. Utapata mimba na kujifungua mtoto mvulana ambaye utamuita Yesu atakuwa mkuu na kuitwa Mwana wa Mkuu zaidi.’ Kulikuwa na kusherehekea sana alipozaliwa Yesu.Ghafla malaika wengi walitoka mbinguni na kuungana kumsifu Mungu. wakasema,’sifa kwa Mungu juu mbinguni na Amani duniani kwa anaowapendelea.’ Wachungaji wakaja kumtembelea na kumuabudu mtoto mchanga mfalme. Walimsifu na kumwabudu Mungu kwa yote walioona na kuskia. Wanaume wa hekima walikuja kutoka mashariki wakimtafuta mtoto Yesu. Nyota ya kung’aa iliwaongoza kwenye giza la usiku ikawaongoza kuja kumheshimu na kumwabudu mfalme wao. Kama Maria, Yosefu, wachungaji na wanaume wa hekima walimsifu na kumtukuza Yesu nasi pia tunapaswa kumsifu na kumtukuza pia. Siku moja tukiwa mbinguni tutakuwa tumeuzunguka ufalme wake tukimwabudu na kumsifu milele na milele.



## UNAWEZA KUFANYA?

- Msifu Mungu kila siku mchana kutwa.
- Msifu Mungu katika kila jambo. Hii ni chaguo lako.
- Kuwa na moyo wa kumshukuru Mungu na wale amewaeka karibu nami: jamii yangu, marafiki na walimu.
- Jifunze tabia ya kusifu.

# Kuabudu

## UCHEZE!

### Wimbo Wangu Pendwa

1. Onyesha na mikono yako mienendo ya nyimbo ya 'nyenyekea machoni mwa Bwana '
2. Angalia kwenye youtube www.youtube.com/watch?v=qpyDJMCL9yc
3. Atakuinua=piga magoti, inua goti moja kisha usimame, halafu nyoosha mikono juu kwa kuabudu Bwana.)
4. Wagawanye wachezaji kwa vikundi viwili na kila kikundi uwapatie nyimbo moja kusikiza kisha watunge mienendo ya mikono (kuwa na nyimbo za kuabudu uzipendazo zaidi tayari)
5. Waache kila kikundi wajifunze mienendo yao na kuwachezea kikundi hicho kingine, kisha watafundishwa wenzao na kuwachezea.
6. Wakimaliza, wachezaji wote wapigie kura nyimbo waliopenda ya kusifu kati ya hizo tatu walizo shuhudia. Baada ya kura waulize "Mbona hiyo ndiyo mnayoipenda?"

- **Ukweli na Uhusiano na maisha: watoto wanajifundisha kuabudu jinsi inamaana kwao naya muhimu-watoto wanatafakari na kufikiria,'nyimbo yangu niipendayo ya kuabudu ni ipi na kwa nini?" Kocha atawaeleza watoto anapenda nyimbo ipi na kwanini**

## MASWALI

1. Kwenye mchezo kwanini ulichagua nyimbo Fulani ya kuabudu? (La dharura: chukua wakati kujiiuliza swali la kwa nini, hii inafanya watoto kufikiria kwa makini swala la kuabudu na kwanini wanapenda kuabudu na nyimbo gani ya kuabudu wanapenda Zaidi).
2. Kwenye bibilia Mungu alimtuma mwanawe Yesu, kisha wachungaji, wanaume wa hekima na hata wafalme wakamuabudu Yesu.Ni wakati upi wa maisha ya Yesu unashukuru zaidi kwa maisha yako, kuzaliwa kwake, kifo chake kulipia dhambi zangu au ufufuko wake?
3. Mpendwa Yesu asante kwa kuja katika umbo la mtoto. Asante Yesu kwa kuwa mwokozi wangu na kufa kulipa adhabu yangu. Yesu nionyeshe njia zingine amabazo ninaweza kukuabudu isipokuwa nyimbo  za kuabudu. (Tulia) Yesu nisaidie niweze kuambia wengine juu ya matendo yako za ajabu kupitia maneno yangu, matendo yangu, na mitazamo yangu.

©2018 cha Agano la Maombi Kwa Watoto / Michezo iliyotolewa na GameLife77.com. Haki zote zimehifadhiwa.



# Kuabudu

## KAZI YA KARATASI

**1** Je unakumbuka mstari wa 5 wa maombi, KUABUDU? iandike hapo chini.

**2** Jaza mapengo.

Zaburi 9:1: Nita ________________ kwa________________ wangu wote,

nitayasimulia ________________ matendo yako yote.

**3** Unaweza kutaja njia tofauti ya kumuabudu Yesu?

**4** Ni njia ipi uipendayo ya kuabudu?

**5** MUDA WAKUJIBU:

Kutengeneza chombo cha muziki ni rahisi na raha. weka kwenye chupa mchele au maharagwe yaliokauka kama nusu. Ipambe chupa na vijiti au kalamu za rangi. Mwimbie na kumchezea Yesu.

# Kuabudu

## NI WIMBO WA




**Yesu anastahili sifa yangu!**

**AMINA, AMINA!**

**Tumsifu kila siku mchana kutwa!**

**AMINA, AMINA!**

**Inamletea furaha akiskia watoto wakimuimbia!**

**AMINA, AMINA!**

**Wote kwa pamoja tuache sifa zake zilie!**

**AMINA, AMINA!**

**Yesu alikuja kutuokoa kutoka dhambi!**

**AMINA, AMINA!**


**Milele tunamuinua kama Kristo Mfalme wetu!**

**AMINA, AMINA!**


Mwalimu anaongoza kwa kusoma maneno ya rangi nyeusi kisha watoto watamjibu na maneno ya rangi ya samawati.Baadae wahimize darasa waandike muziki wa rap kama kikundi,wakiandika fikira zao kwenye ubao. Waangalie watakavyo kuwa na furaha wanapo imba walichoandika.

# Kujitolea

*Yesu nataka kukufuata*
*kama mwokozi wangu.*
*Nibadilishe upendavyo.*



Petero hakuwa mwema • Luka 22:54-62



## LUKA 9:23

**Anayetaka kuwa mfuasi wangu lazima ajinyime na kuchukua msalaba wake wa kila siku anifuate.**



# Kujitolea

## UNAWEZA KUIPATA?

*Yesu nataka kukufuata kama mwokozi wangu. Nibadilishe upendavyo.*

**LUKA 9:23**

Anayetaka kuwa mfuasi wangu lazima ajinyime na kuchukua msalaba wake wa kila siku anifuate.

## UNAWEZA KUIPATA?

*Mathayo 4:18-22*

*Mathayo 16:24*

*Wagalatia 2:20*

## UNAIHISI?

Inamaanisha nini kumfwata Yesu?

Mungu ananibadilishaje?

Nani au nini unajitolea kufuata?

# Kujitolea

## "AINA YA MAOMBI POPCORN" KIPINDI CHA KUJADILIANA

Ongoza watoto kwa maombi wakisema, ***"Yesu nataka kukufuata kama Bwana Mwokozi wangu, nibadilishe upendavyo."*** Washawishi watoto warudie ombi. Wahimize kuomba sentensi moja wakisema jinsi wanataka kumfuata Yesu kama mwokozi wao. Wanaweza kutaja majina tofauti ya Mungu au sifa zake kama ilivyo tumika kwenye somo la mfano.

## IONGEE!

- Kujitolea ni ahadi ya uaminifu kwa mtu au kitu.
- Kujitolea inatumia wakati wako, pesa na ni kazi ngumu. Ni kama kuwa mchezaji wa kikosi cha michezo ambapo unalipa karo, unaenda mazoezi kisha kujitokeza kwenye michezo.
- Yesu anataka ujitole kumufuata kama mwokozi wako.
- "Nibadilishe upendavyo" ni kusema uko tayari kujitolea kikamilifu maisha yako kwa Kristo.
- Kujitolea sio rahisi.

Unapoongea juu ya kujitolea, waache watoto wakueleze wamejitolea namna gani (kwenye michezo, muziki na kadhalika) na ni nini ngumu na rahisi kuweza kujitolea. Ongea nini maana ya kujitolea kuwa mfuasi wa Yesu. Ni njia gani zina usawa au utofauti. wahimize waongee na uhuru na ukweli kiwazi.

# Kujitolea

## UNAWEZA KUISIKIA?

**Petero hakuwa mwema (Luka 22:54-62)**

Petero wakati mmoja alimwambia Yesu. "Hata wengine wote wakikukana, mimi sitafanya hivyo!" Yesu alijua tofauti akamwambia Petero kabla jogoo kuwika atamkana mara tatu kwenye baraza la wakuhani wakuu ambapo Yesu alikuwa akihojiwa kabla ya kusulubishwa. lilitendeka kama alivyosema. Msichana mmoja mfanyakazi alimuona Petero akasema, "Ulikua na Yesu." "La, hiyo sio ukweli-sijui unaongea kuhusu nini" kisha Petero akamkana Msichana mfanyakazi mwengine akawaambia watu waliokuwa hapo,'Huyu mtu alikuwa na Yesu,'Petero akakana tena Muda kiasi ukapita Petero alikuwa ana wasiwasi na uwoga sana. Alitaka watu waache kumtambua ila ikafanyika tena "tunajua ummoja wao, unaongea kama mtu kutoka Galilaya". Petero akaanza kulaani na kutoka jasho akasema "simjui mtu huyo." Kisha ikafanyika alivyosema Yesu, jogoo likawika "kuku-ru-kuuuu!" Ghafla Petero akakumbuka maneno ya Yesu, akakimbia akilia. Alifahamu amefanya kabisa alichosema Yesu akajihisi vibaya sana. Lakini Yesu hakumwacha Petero, baadae alipofufuka alikuwa kwenye ufuo wa ziwa tiberias akipata kiamsha kinywa na wafuasi Yesu akamuuliza Petero mara tatu, "Je Petero wanipenda?" Na kila wakati akamjibu "Ndiyo Bwana, unajua nakupenda". Na kila wakati Yesu alimwambia "waliishe kondoo wangu". Yesu alitaka Petero awe mfuasi wake na kufanya wengine wawe wafuasi. Ingawaje Petero hakuwa mwema, Yesu alijua Petero alitamani sana kumufuata kama mwokozi wake, Petero hakuwai mkana Yesu tena



## UNAWEZA KUFANYA?

- Kujitolea kumufuata Yesu kama mwokozi wa maisha yako
- Kujitolea na kumuacha Yesu atawale fikira, mienendo na mapenzi yako
- Mjulishe Yesu ana thamani kubwa sana kwako kuliko chochote duniani na unataka kumufuata, kumtii na kuwa kama yeye

# Kujitolea

## UCHEZE!

### Kweli au Uwongo

1. Wachezaji wote wapange mstari katikati ya chumba, kisha wasimame wakiangaliana migongo
2. Tengeneza mstari ukigawanya chumba kwa nusu, upande wa kulia na kushoto, waeleze utawauliza swali ambayo watajibu kweli au uwongo, lakini badala ya kujibu kwa kusema, “Kweli” au “Uwongo” watakimbia kulia kwa jibu la kweli na kushoto kwa uwongo
3. Maswali yanaweza kuwa ya kufurahisha kama ‘Mwezi umetengenezwa na jibini ya manjano!’ (Jibu lake ni uwongo kwa hiyo wachezaji wanapaswa kukimbia kushoto)
4. LA KUFURAHISHA: Wachezaji wawili wa mwisho kufika ukutani wametolewa na wataketi hadi mchezo ufuatao. Endelea na mchezo hadi wane wa mwisho, hao ndiyo “Washindi wa Ukweli”
5. DHARURA: Waulize maswali kutoka vipindi vya awali. “Yesu mchungaji mwema hakupoteza kondoo yeyote!” (Jibu ni ukweli kwa hiyo wachezaji wakimbie kuelekea “ukuta wa kulia”)

- **Ukweli na Uhusiano na maisha: Petero hakusema ukweli, alisema uwongo kujikinga na alijihisi vibaya kwa kusema uwongo. Mungu anataka tuseme ukweli kila wakati.Yesu ndiye njia, ukweli na uzima. Waumini wanapaswa kujitolea kufuata na kutii ukweli**

## MASWALI

1. Kwenye mchezo kuna majibu mawili peke yake kwa kila swali, “Ukweli” au “Uwongo”. Ulikimbia upande gani wakati jibu lilikuwa ukweli (kulia)
2. Kwenye bibilia Petero alisema ukweli au uwongo? kwa nini alisema uwongo? Ukiwa na uchaguzi wa kusema ukweli au uwongo, unapaswa kufanya nini? (sema ukweli) kwa nini? (uwongo unafanya tujihisi vibaya na kusema uwongo ni kutomtii Mungu)
3. Yesu Mpendwa nataka kukufuata kama mwokozi wangu. Nibadilishe upendavyo. Yesu nionyeshe njia za kukufuata (tulia) Njia inaweza kuwa ngumu lakini nakuamini kuniongoza.

©2018 cha Agano la Maombi Kwa Watoto / Michezo iliyotolewa na GameLife77.com. Haki zote zimehifadhiwa.



# Kujitolea

## KAZI YA KARATASI

❶ **Je unawezakumbuka mstari wa 6 wa maombi, KUJITOLEA? liandike hapo chini.**

❷ **Jaza mapengo.**

**Luka 9:23: Ye yote anayetaka _____________ ni lazima ajikane _____________**

**yake, achukue _____________ wake kila siku _____________ .**

❸ **Kwa nini kumfuata Yesu ni kujitolea?**

❹ **Ni vitu kama vipi umejitolea?**

❺ **MUDA WAKUJIBU:**

**Funga macho kisha umuulize Yesu na usikize, “Ningekuaje kama ningekufuata kwa kujitolea na mapenzi makubwa?” Unge kuwa una fanya nini? Chora picha Yesu amekuonyesha na waonyeshe wanafunzi wenzako na wazazi wako.**

# Kujitolea

## NI WIMBO WA




**Unamsaidia mama yako na kazi siku nzima.**

**NI VYEMA! NI VYEMA!**

**Unajiunga na kikundi cha michezo nakusahau kwenda michezoni.**

**NI VIBAYA! NI VIBAYA!**

**Unamsaidia rafiki yako anayehangaika darasani.**

**NI VYEMA! NI VYEMA!**

**Unaamua kutohudhuria masomo yako ya kinanda, unataka tu uzembe.**

**NI VIBAYA! NI VIBAYA!**

**Unaweka ahadi zote ulizofanya.**


**NI VYEMA! NI VYEMA!**

**Kwa hiyo weka ahadi zako na ukumbuke kuomba!**

Mwalimu anaongoza kwa kusoma maneno ya rangi nyeusi kisha watoto watamjibu na maneno ya rangi ya samawati.Baadae wahimize darasa waandike muziki wa rap kama kikundi,wakiandika fikira zao kwenye ubao. Waangalie watakavyo kuwa na furaha wanapo imba walichoandika.

# Kutegemea

*Nijaze na Roho Mtakatifu.*
*Nataka kujua mipango yako kwangu.*





WAEFESO 5:18b

Bali mjazwe Roho.



# Kutegemea

## UNAWEZA KUIPATA?

*Nijaze na Roho Mtakatifu. Nataka kujua mipango yako kwangu.*

**WAEFESO 5:18b**
Bali mjazwe Roho.

## UNAWEZA KUIPATA?

*Matendo 2:1-17*

*Warumi 8:26,27*

*Warumi 15:13*

*Wagalatia 5:22-26*

*Yohana 16:13a*

## UNAIHISI?

Unamanisha nini kujazwa na Roho?

Inamaanisha nini kumtegemea Mungu?

Inamaanisha nini kuisikia sauti ya Mungu?

Tunawezaje kujazwa na Roho?

# Kutegemea

## "AINA YA MAOMBI POPCORN" KIPINDI CHA KUJADILIANA

Waongoze watoto kwenye maombi wakisema ***"Nijaze na Roho Mtakatifu, nataka kujua mipango yako kwangu."*** Waache watoto warudie ombi hilo. Washawishi kuomba sala ya sentensi moja wakimuomba Mungu awajaze Roho na kuwafanya chombo ambacho Roho atapitia. Wanaweza kutaja majina ya Mungu tofauti au sifa zake.

## IONGEE!

- Mungu anataka kuongea nasi. Mara nyingine ni vigumu kumskia, lakini tukiendelea kusikiliza tutajifunza kujua sauti yake.
- Tunahitaji kutegemea Roho Mtakatifu. Tunahitaji kutegemea nguvu za Mungu na sio zetu.
- Tunahitaji kutegemea Roho yake ili tuwe kama Yesu.Tunahitaji kutegemea nguvu za Mungu na sio zetu wenyewe.
- Ukijazwa na Roho, Yesu ataweza kukutumia zaidi na zaidi.
- Utakuwa na upendo, furaha, amani, utulivu na matendo mengine ya Roho zaidi.

Ongoza mazungumzo kwa kuwaeleza inamaanisha nini kuwa na rafiki na mfariji ambaye unamtegemea kukusaidia na kukuongoza kila siku. uhusiano huo ukoje? Ongeeni kuhusu matunda tofauti ya Roho na waache watoto wakuambie zipi ni changamoto kwao zaidi ya zingine.

# Kutegemea

## UNAWEZA KUISIKIA?

**Mfariji (Yohana 14:15-31)**

Chukua muda na ufunge macho, mfikirie rafiki umpendaye zaidi. Unaona uso wao? Sasa mfikirie akisema, "naondoka kesho kwenda sehemu ya mbali sana, mahali huwezi kwenda. Lakini usitie shaka, ntakuachia Roho yangu kuongea na kucheza na wewe." Jambo hili haliwezi fanyika nje ya Mungu lakini ndicho kilichofanyika kabla Yesu afe msalabani na kufufuka mkono wa kulia wa Baba mbinguni. Hakutuwacha peke yetu,Yesu alisema kwa Yohana 14:16-17, "Nami nitamuomba Baba, naye atawapeni Msaidizi mwingine akae nanyi siku zote. Huyo ndiye Roho wa Kweli."



Yesu alimtuma Roho kusaidia na utume wa kanisa. Haikua muda mrefu baada ya hapo siku ya Pentekoste upepo mkali ulivuma, ukajaza kila mtu na Roho Mtakatifu. Roho atakaa nao kila wakati kama mfariji, mwalimu na kiongozi. Roho Mtakatifu huyo anakaa ndani ya wale wajiitao watoto wake kama wewe na mimi anataka kutuongoza na Roho. Tunamskiza?

## UNAWEZA KUFANYA?

- Mtegemee Roho wa Mungu akuongoze, akufariji na kukufundisha.
- Muombe Baba wa mbinguni kila siku akujaze na Roho.
- Naweza kuchukua muda kusikiza Mungu? Mpe Mungu pongezi! inamaanisha kutulia kabisa dakika tano na Mungu mkuu. Kusikiza ina maana zaidi ya kuongea. Mungu anaweza kuongea na wewe kivipi? Soma Zaburi 46:10 pamoja

# Kutegemea

## UCHEZE!

### Simon Anasema

1. Kabla ya kuanza mchezo waeleze wachezaji wasikize maagizo vizuri.
2. Kocha wa mchezo ni Simon. Anawapa maagizo kama "shika vidole vya miguuni"' watoto wanapaswa kutenda iwapo tu watambiwa Simon amesema.
3. Watoto watatolewa wakifanya kitendo ambacho Simon hakuwaambia.
4. Mwanzoni kila maagizo Simon atawambia watoto yawe rahisi kufuata. Kwa mfano, shika sikio, ruka mara tano, lalia tumbo, keti chini, simama. Mchezo unapoendelea Simon atawapa maagizo magumu zaidi kama Simon amesema gusa vidole vya miguu na sio pua, Simon amesema gusa pua na vidole vya miguu. 'gusa masikio (bila kusema simon amesema)
5. Cheza hadi wabakie wachezaji wanne na uwatangaze washindi wa kusikiza na kufuata.
6. DHARURA: Cheza tena wakati huu Simon atoe maagizo KWA SAUTI YA CHINI.
7. Cheza hadi wabakie wachezaji wanne na uwatangaze washindi wa kusikiza na kufuata.

- **Ukweli na Uhusiano na maisha: Mungu anasema nasi kila wakati kupitia Roho mtakatifu. Lazima tutegeme na kuamini Mungu atatufariji, kutufundisha na kutuongoza. Tunapaswa kuwa makini kusikiliza Mungu akisema.**

## MASWALI

1. Kumtii Simon ilibidi ufanye nini? (kuskiza kwa makini, na kutii amri ya Simon)
2. Tunapaswa kumskia Roho Mtakatifu wa Mungu, mfariji, mwalimu na kiongozi. Tunawezaje kuskia Mungu akiongea nasi? Tufanyeje? (skiza kwa makini, kutii haraka amri kutoka Mungu) inamaanisha nini kumtegemea, kumuamini na kukubali Roho mtakatifu kutuongoza?
3. Mungu nijaze na Roho Mtakatifu, nisaidie kuskiza sauti yako ya chini unapo ongea nami. Roho mtakatifu ongea na moyo wangu na nionyeshe njia ya kukufuata zaidi (tulia)Roho Mtakatifu asante kuwa mwalimu na kiongozi wangu.

©2018 cha Agano la Maombi Kwa Watoto / Michezo iliyotolewa na GameLife77.com. Haki zote zimehifadhiwa.



# Kutegemea

## KAZI YA KARATASI

1. **Inazidi kuwa ngumu lakini utaweza. Je unakumbuka mstari wa 7 wa maombi KUTEGEMEA? Iandike hapo chini.**

2. **Jaza mapengo.**

   **Waefeso 5:18b: Bali __________________ __________________**

3. **Taja matunda ya Roho Mtakatifu:**

   __________________ __________________ ____________________

   __________________ __________________ ____________________

   __________________ __________________ ____________________

4. **Ni tunda lipi gumu sana kwako kutekeleza? Kuomba kutasaidia kivipi?**

5. **MUDA WAKUJIBU:**

   **Mpe Mungu pongezi! Funga macho na skiza Mungu anaweza kuwa akikuambia nini. Alikukumbusha aya ya bibilia? Alikupa fikra yeyote? Amekukumbusha mtu yeyote haswa? Chora kwenye karatasi au andika unachofikiria Mungu anakuambia.**

# Kutegemea

## NI WIMBO WA




**Katie aliamua kumwalika rafiki yake kanisani.**

**NDANI YA ROHO? NDIYO, NDIYO, NDIYO!**

**Joe hakusomea mtihani akadanganya.**

**NDANI YA ROHO? APANA, APANA, APANA!**

**Suzie alitoa ushuhuda kwa darasa lake nzima.**

**NDANI YA ROHO? NDIYO, NDIYO, NDIYO!**

**Brian alimfundisha dada yake kuendesha baiskeli.**

**NDANI YA ROHO? NDIYO, NDIYO, NDIYO!**

**Peter alichukua kitu kisicho chake.**

**NDANI YA ROHO? APANA, APANA, APANA!**

**Jesse aliaanza kumuombea mtoto wa mmshionari.**

**NDANI YA ROHO? NDIYO, NDIYO, NDIYO!**

Mwalimu anaongoza kwa kusoma maneno ya rangi nyeusi kisha watoto watamjibu na maneno ya rangi ya samawati.Baadae wahimize darasa waandike muziki wa rap kama kikundi,wakiandika fikira zao kwenye ubao. Waangalie watakavyo kuwa na furaha wanapo imba walichoandika.

# Ushawishi

***Nifanye chombo cha neema,***
***ukweli na haki.***



**Yesu na watoto • Mathayo 18:1-6**



## YOHANA 1:14

**Tumeuona utukufu wake, utukufu wa Mwanae pekee, aliyetoka kwa Baba aliyejaa neema na ukweli.**



# Ushawishi

## UNAWEZA KUIPATA?

*Nifanye chombo cha neema, ukweli na haki.*

**YOHANA 1:14**

Tumeuona utukufu wake, utukufu wa Mwanae pekee, aliyetoka kwa Baba aliyejaa neema na ukweli.

## UNAWEZA KUIPATA?

*Mathayo 19:13-15*

*Matendo 2:16,17*

*Luka 18:15-17*

## UNAIHISI?

Ni zawadi zipi Mungu amenipa?

Nawezaje kuonyesha neema ya Mungu kwa wenzangu?

Tofauti ya ukweli na uwongo ni nini?

Kuna kosa kudanganya?

# Ushawishi

## "AINA YA MAOMBI POPCORN" KIPINDI CHA KUJADILIANA

Waongoze watoto kwenye maombi wakisema ***"Nifanye kuwa mtume wako wa neema, ukweli na haki."*** Waache watoto warudie ombi hilo. Washawishi kuomba sala ya sentensi moja wakimuomba Mungu kuwatumia kueneza ukweli wake, kuonyesha neema kwa wenzao. Wanaweza kutaja majina ya Mungu tofauti au sifa zake.

## IONGEE!

- Yesu alionyesha uhaki kila siku alipo ponya wagonjwa na kusaidia maskini.
- Hakujali kama walikua wazee, wachanga, tajiri au maskini.
- Aliwafanyia wote sawa.
- Aliwaonyesha wote upendo na neema.
- Aliongea ukweli kila wakati.

Waache watoto waseme jinsi wanaweza kuwa watume wa haki. Mjadiliane wakati gani inaweza kuwa mgumu kusema ukweli. Kuficha neno la Mungu moyoni mwako itakusaidia kivipi kuongea ukweli?

# Ushawishi

## UNAWEZA KUISIKIA?

**Yesu na watoto (Mathayo 18:1-6)**

Mchana mmoja mwema wa jua la kuwaka vizuri, wafuasi walikua wameketi wamemzunguka Yesu. Kama tunavyowaza nani anatendewa vizuri nyumbani, shule au kwenye uwanja wa michezo, wafuasi pia walifikiria hivyo. Yesu wakamuuliza wakijikuna vichwa, "nani kati yetu ni bora zaidi kwenye ufalme wa mbinguni?" Fikira zangu nikuwa walidhani Yesu atataja mmoja wao. Yesu alijua walichofikiria na akaita mtoto aje. "Simama kando yangu" akasema. Kisha akawatazama machoni wafuasi wake na kusema kitu cha ajabu. "Yeyote atakaye nyenyekea kama huyu mtoto ndiye bora zaidi kwenye ufalme wa mbinguni." Akaendelea akisema kitu cha ajabu zaidi "yeyote atakaye mkaribisha mtoto mdogo kwa jina langu ananikaribisha". Na unajua kama Yesu alisema hivyo, aliimanisha hivyo kwa sabau aliongea ukweli peke yake.



Yesu alikua na moyo wa haki. Aliwajali maskini. Aliwaonyesha huruma wagonjwa. Aliwaletea amani waliokuwa wanumia kindani, pia alipenda kutumia muda wake na watoto ambao mara nyingi walisahauliwa. Yesu alisema, "itakuwa vibaya sana kwa mtu atakaye muumiza mtoto mdogo" unaona jinsi Mungu anakupenda na kukujali?

## UNAWEZA KUFANYA?

- Mruhusu Mungu akutumie kwa ujumbe wa neema, ukweli na haki.
- Amua moyoni mwako kuongea ukweli kila wakati.
- Jifunze kukariri neno la Mungu.

# Ushawishi

## UCHEZE!

### Hapa kuna Adhabu NA Habari Njema Ya Vitendo Vya Mikono

1. Wachezaji wote wanapanga mstari upande mmoja wa chumba au kwenye uwanja. Waonyeshe mahali umbali kiasi watakapofika. waambie wachezaji watakimbia kutoka (mwanzo wa mstari) hadi (umbali kiasi) kisha warudi.

2. DHARURA: Weka umakini kwa muda wachezaji wanatumia kukimbia hadi kurudi kwa mstari wa kuanzia. Watakimbia tena na wakati huu watumie muda nusu ama kuna adhabu ya kujishinikiza juu mara 10.
   DHARURA: Kwa zoezi hili wachezaji HAWAWEZI kumaliza kwa muda huo kwa hiyo shindano hili limetengenezwa ili wachezaji washindwe.

3. Waache wachezaji kujaribu tena. Waruhusu wasichana peke yao wakimbie, waruhusu wavulana peke yao wakimbie hata wachezaji wadogo pia waruhusiwe kukimbia peke yao.

4. Baada wachezaji wamejaribu mara nyingi kwa masikitiko hawataweza kukamilisha lengo lao. wameshindwa na lazima kuwe na adhabu kwa kutotimiza lengo.

5. Kabla ya wachezaji kupewa adhabu za kujishinikiza juu - moja wa kocha aje awaambie: “Kocha huwezi kuwafanya hawa wachezaji kujishinukiza juu! Ona walivyochoka.” Utajibu: Ndiyo lakini tulikubaliana kutakua na adhabu. Kisha kocha mwengine aseme: “Ngoja, nitawalipia adhabu” (kabla kuwe na mazungumzo zaidi kocha huyo mwengine atanza adhabu ya kujishinikiza mara 10).

6. Wafanye watoto wahesabu hizo shinikiza za juu wakati kocha anaifanya adhabu hiyo Wakihesabu 1-2-3-4-5-6-7-8-9-10!

7. Waonyeshe na uwafundishe jinsi ya kufanya “Creation To Christ Hand Motions” (Tazama ukurasa wa kiambatisho kwa picha za huu mchezo).

- **Ukweli na Uhusiano na maisha: Mungu anapendelea kutumia watoto kuhimiza jamii na marafiki wao.**

## MASWALI

1. Wavulana na wasichana mikono yenu imechoka kwa kujishinikiza juu? (Hapana, kocha alitufanyiwa adhabu) Wah! Ni kwa nini Kocha aliwafanyia adhabu?
2. Kwa bibilia kwa sababu ya dhambi zetu, vitu ambavyo havikumfurahisha Mungu, tulipaswa kupata adhabu (kifo) nani alitulipia adhabu? (Yesu) kwanini Yesu atulipie adhabu?
3. Yesu asante kwa kunipenda sana hadi ukafa kwa nafasi yangu, ulichukua adhabu yangu. Wavulana na wasichana tukae kimya kwa muda na kufikiria Yesu anavyotupenda. (Tulia) Yesu tafadhali nisamehe makosa yangu. Nataka kutubu na kugeuka kutoka dhambi zangu. Yesu tafadhali uwe Mwokozi wangu. Yesu maisha yangu yataonyeshaje neema, ukweli na uhaki? (Tulia) Yesu asante kunifanya mmoja ya watoto wako. Roho Mtakatifu ng’ara ndani yangu kila wakati na kila siku.



©2018 cha Agano la Maombi Kwa Watoto / Michezo iliyotolewa na GameLife77.com. Haki zote zimehifadhiwa.



# Ushawishi

## KAZI YA KARATASI

1. Unakumbuka mstari wa 8 wa maombi SHINIKIZO, na uiandike hapa chini?

2. Jaza mapengo.

   Yohana 1:14: Nasi tumeuona utukufu wake yeye aliyemwana wa peke wa ____________

   amejaa ____________ na ____________.

3. Umemkaribisha mtu aliyekuwa mgeni shuleni, kanisani ama ujirani kwenu? Kama umefanya hivyo, tuambie ulimkaribisha lini. Kama bado, mbona usijaribu? Ukiifanya sana inakua rahisi.

4. Unaweza kufikiria ulipomshawishi mtu kufanya wema kwa wakati mgumu? Kama ndiyo, huyo mtu aliitikaje kwa usaidizi wako?

5. MUDA WAKUJIBU:

   Muulize Mungu kisha usikize unapojibu maswali. Unaweza kufikiria jinsi Mungu anakutumia kufikia watu waliokaribu na wewe? Labda uanzishe kikundi cha kuomba kanisani. Labda alika marafiki kanisani ambao kawaida hawaendi kanisani. Mkaribishe jirani mgeni au mtoto darasani,

# Ushawishi

## NI WIMBO WA




**Nataka kua mtumishi wako wa ukweli!**

**NDIYO, NDIYO!**

**Nataka kusema maneno yako ya neema!**

**NDIYO, NDIYO!**

**Nataka kuonyesha haki yako maishani mwangu kila siku!**

**NDIYO, NDIYO!**

**Nataka kuwasaidia waliopotea na kuenda pabaya!**

**NDIYO, NDIYO!**

**Nataka kusaidia wasio na chochote!**

**NDIYO, NDIYO!**

**Nataka kusaidia wasiotambuliwa!**


**NDIYO, NDIYO!**

**Nataka kuwa mtume wako wa upendo!**

Mwalimu anaongoza kwa kusoma maneno ya rangi nyeusi kisha watoto watamjibu na maneno ya rangi ya samawati.Baadae wahimize darasa waandike muziki wa rap kama kikundi,wakiandika fikira zao kwenye ubao. Waangalie watakavyo kuwa na furaha wanapo imba walichoandika.

# Ufuasi

***Nitumie kwa utukufu wako niweze kualika wengine wakufuate***



Saulo wa Tarsus ageuka kuwa Paulo mtume wa Yesu Kristo • Matendo 9:1-22



## MATHAYO 28:19

**Nenedeni basi mkawafanye watu wa mataifa yote wawe wafuasi wangu, mkiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu.**



# Ufuasi

## UNAWEZA KUIPATA?

*Nitumie kwa utukufu wako niweze kualika wengine wakufuate.*

**MATHAYO 28:19**

Nenedeni basi mkawafanye watu wa mataifa yote wawe wafuasi wangu, mkiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu.

## UNAWEZA KUIPATA?

*Marko 16:15*

*Yohana 17:4-5*

*Warumi 10:13-17*

*Wakolosai 3:17*

## UNAIHISI?

Mmishonari ni nani

Mfuasi ni nani?

Tunaweza kutumia njia gani kuwaambia wengine kuhusu Yesu?

Inamaanishaje kufanya kitu kwa utukufu wa Mungu?

# Ufuasi

## "AINA YA MAOMBI POPCORN" KIPINDI CHA KUJADILIANA

Waongoze watoto kwenye maombi wakisema ***"Nitumie kwa utukufu wako niweze kuwaalika wengine wakufuate."*** Waache watoto warudie ombi hilo. Washawishi kuomba sala ya sentensi moja wakimuomba Mungu awatumie kwa utukufu wake na umairifu kualika wengine kumfuata Yesu. Wanaweza kutaja majina ya Mungu tofauti au sifa zake zilizofunzwa kwenye somo.

## IONGEE!

- Wamishonari ni wale wameitwa na Mungu kueneza injili ya Yesu Kristo.
- Mara nyingi inamaanisha wanasafiri kwa nchi za mbali na kwenda kujifunza lugha na tamaduni mpya. Ni maisha ya kujitolea na kujinyima kumtukuza Mungu.
- Yesu anataka wote tuwe mamishonari popote tunapoishi na kuwa mwanga wake shuleni na hata nyumbani.

Unaweza kuanza na kuaalika watoto waongee kuhusu hadithi za mishionari kutoka kanisa lao au wanowajua duniani. Wahimize kuongea jinsi wanaweza kueneza Yesu kwa jamii na marafiki wao.

# Ufuasi

## UNAWEZA KUISIKIA?

**Saulo wa Tarsus ageuka kuwa Paulo mtume wa Yesu Kristo (Matendo 9:1-22)**

Paulo wakati mmoja aliyechukia sana na kuwa adui wa Kristo na wafuasi wake alikuja kuwa mmoja wa viongozi muhimu sana kwenye kanisa la mwanzo na mmishonari wa injili. Ilifanyika siku moja wakati Saulo (kabla jina lake halijabadilishwa kuwa Paulo) alikuwa anatembea barabarani akielekea Damascus. Mwanga mkali kutoka mbinguni ukamfanya akaanguka chini. Ikamfanya kipofu. Saulo akasikia sauti ikisema, "Saulo mbona wanitesa?" "Wewe ni nani Bwana?" Saulo akauliza. "Mimi ni Yesu ambaye unamtesa". Saulo aliogopa na kutetemeka. Kwa siku tatu hakuweza kuona wala kula na kunywa. Mtu aitwae Ananias mcha Mungu alitumwa na Mungu aende akamtafute Saulo. "Aanias,'nataka umrudishie Saul uwezo wa kuona. Nimemchagua kuwa mumishonari wangu." Hii haikueleweka na Ananias. Alikuwa ameskia vitu vyote vibaya Saulo alifanya kwa wakristo lakini Ananias alimtii Mungu. Mungu akamponya Saulo, na Saulo akaanza kuhubiri na kufundisha kuhusu Yesu kila alipokwenda. Wengi wakawa wafuasi wa Yesu. Jina Saulo baadae likabadilishwa kuwa Paulo. Bibilia imejaa mafunzo ya Paulo na barua zake kwa makanisa. Alibadilisha dunia juu chini kwa sababu ya Yesu, akimpa utukufu wote Mungu nakufundisha wengine wafanye hivyo pia.



## UNAWEZA KUFANYA?

- Amua moyoni chochote utakachofanya, utafanya kumtukuza Mungu.
- Tambua talanta na uwezo wako vyote vinatoka kwa Mungu
- Wacha vyote utakavyo fanya iwe zawadi kwa upendo wa Yesu.
- Mwambie Mungu akupe umahiri wa kualika wengine kumfuata.
- Muombe Mungu nafasi ya kutangaza upendo wake popote unapoenda. Unaweza kupata zana hii ya furahisha na rahisi kujifunza kwenye ukurasa wa 109 nyuma ya kitabu hiki

# Ufuasi

## UCHEZE!

### Kushikana kwa wavu

1. Waonyeshe wachezaji mipaka mchezo utakapo chezwa.
2. USALAMA: Kama kuna wachezaji wengi wagawanye kwenye vikundi vingi na wachezaji wadogo upande mmoja na wakubwa wakichezea upande mwingine.
3. DHARURA: Waeleze mchezo hautaisha mpaka wachezaji wote wamenaswa kwenye wavu
4. DHARURA: Mchague mchezaji mdogo zaidi na mwengine kutoka kikundi kile kingine. huyo mchezaji anawakimbiza wenzake akijaribu kuwashika na wengine wajaribu kutoroka.
5. Atakaye shikwa wanashikana mikono na waote sasa watakuwa wavu.
6. Kila mchezaji ashikwae anajiunga na hawa ambao sasa wamekuwa wavu, wakishikana mikono kwa mstari.
7. Endeleeni kucheza hadi 'wavu'ishike wachezaji wote.
8. Endeleeni kucheza raundi nyingine vile muda utawaruhusu, kila wakati mchezaji mdogo akiwa wakuanza kushika wenzake.

- **Ukweli na Uhusiano na maisha: Mchezaji mmoja akianza kwa kushika mchezaji mmoja, Kisha wavu inakua mkubwa na kushika wengine hadi wote wameshikwa kwenye wavu. Ufuasi unaanza na mtu tu mmoja kisha unaongezeka kwa watu wengi.**

## MASWALI

1. Kwenye mchezo watoto wangapi walishikwa kwenye wavu ndo mchezo uishe, watatu au wanne? (kila mtu!) Ngoja, mchezaji mmoja aliwezaje kushika kila mtu kwenye wavu? (ilianaza na mmoja kisha ikaongezeka)
2. Kwenye Bibilia Yesu aliwaambia wafuasi wake wafanye nini? Je aliwaambiwa wafanye wafuasi wa taifa moja peke yake? (la, mataifa yote!)
3. Mpendwa Yesu nataka kukutii kwa kufanya wafuasi kwa mataifa yote. Naweza kuanza leo saa hii kwa kuombea mataifa yote na kuambia kila mtu namjua kukuhusu. Mungu nionyeshe saa hii watu unataka niwasii wakufuate (tulia)Yesu nifundishe kuwa wakuleta wafuasi vizuri.

©2018 cha Agano la Maombi Kwa Watoto / Michezo iliyotolewa na GameLife77.com. Haki zote zimehifadhiwa.



# Ufuasi

## KAZI YA KARATASI

1. Karibu tunamaliza! Unakumbuka mstari wa 9 wa maombi, UFUASI, na uiandike hapo chini?

2. Jaza mapengo.

   Mathayo 28:19: Nendeni mkawafanye _________________ yote kuwa _________________

   wangu mkiwabatiza kwa _________________ na la _________________ na la

   Roho _________________.

3. Mmishonari ni nani?

4. Mimi na wewe tunawezaje kuwa mmishonari na kuwafanya wafuasi wenzetu katika ujirani wetu?

5. MUDA WAKUJIBU:

   Mtaje mtu mmoja unayemjua ambaye asiyemjua Yesu. Andika jina lake kwenye kadi kisha jitolee kumuombea kila siku. Kumbuka Mungu anaweza kukutumia kuwaelezea wengine kuhusu pendo lake.

# Ufuasi

## NI WIMBO WA RAP!

**Napenda sana kuwa na moyo wa Mungu kupenda.**

**NDIYO, NDIYO!**

**Napenda sana kuwa na moyo wa Mungu kutumikia.**

**NDIYO, NDIYO!**

**Najua Mungu anaweza kunitumia kama mwana wake mdogo.**

**NDIYO, NDIYO!**

**Kueneza hadithi ya pendo lake lisiloisha.**

**NDIYO, NDIYO!**

**Nataka kwenda kuwafanya wafuasi kwa jina la Yesu.**

**NDIYO, NDIYO!**


**Utanisaidia kwenda kufanya hivyo?**

**NDIYO, NDIYO!**

Mwalimu anaongoza kwa kusoma maneno ya rangi nyeusi kisha watoto watamjibu na maneno ya rangi ya samawati.Baadae wahimize darasa waandike muziki wa rap kama kikundi,wakiandika fikira zao kwenye ubao. Waangalie watakavyo kuwa na furaha wanapo imba walichoandika.

# Mamlaka

***Kwa jina la Yesu nimeomba, Amina.***



**Bartimayo kipofu • Marko 10:46-52**



**WAFILIPI 2:9**

**Kwa sababu hiyo Mungu alimuinua juu kabisa na akampa jina ambalo ni kuu kuliko majina yote.**



# Mamlaka

## UNAWEZA KUIPATA?

*Kwa jina la Yesu nimeomba, Amina.*

**WAFILIPI 2:9**

Kwa sababu hiyo Mungu alimuinua juu kabisa na akampa jina ambalo ni kuu kuliko majina yote.

## UNAWEZA KUIPATA?

*Mathayo 1:21*

*Mathayo 28:18*

*Yohana 14:13*

*Matendo 4:12*

## UNAIHISI?

Nini kingefanyika ungekuwa na mamlaka ya dunia nzima?

Mbona kuna nguvu kwa jina la Yesu?

Mbona ni vyema Yesu anamamlaka ya dunia yote?

Kwanini tuombe kwa jina la Yesu?

# Mamlaka

## "AINA YA MAOMBI POPCORN" KIPINDI CHA KUJADILIANA

Waongoze watoto kwenye maombi kwa kuwashawishi kuomba sala ya sentensi moja wakimuomba katika jina la Yesu. Hii inaweza kua ya uponyaji wao ama mpendwa wao au kuwasaidia kukuwa katika upendo au kutumika na Mungu kwa njia ya kipekee. Wanaweza kutaja majina ya Mungu tofauti au sifa zake kutoka sampuli ya mafundisho.

## IONGEE!

- Bibilia inasema, "Mamlaka yote yamepewa kwangu duniani na hata mbinguni." Tukiomba kwa jina la Yesu tuna mamlaka.
- Hii inaleta maswali: Mungu anajibu maombi yetu yote vile tunataka tukiomba katika jina la Yesu? Inamaanisha Mungu atanipa kila kitu ninataka?
- Maombi yetu yanapaswa kulenga vitu vitakavyomtukuza Baba yetu mbinguni na kueneza ufalme wake duniani.

Waache watoto waongee kiwazi kuhusu maisha yao ya kuomba. Wameshuhudia maombi yakijibiwa? Wamefadhaika walipoona maombi yao hayakujibiwa walivyotaka au hata kutojibiwa kabisa?

# Mamlaka

## UNAWEZA KUISIKIA?

**Bartimayo kipofu (Marko 10:46-52)**

Bartimayo alikuwa kipofu na ombomba aliyeishi mitaani Jericho.Alijua kuhusu Yesu na matendo yake mema. Alikuwa ameskia jinsi Yesu aliponya wagonjwa, vipofu waliona na walemavu walitembea. Bartimayo alitaka Yesu amponye pia. Akalia "Yesu, Bwana wangu nionee huruma" Watu waliokuwa karibu naye hawakuwa wakarimu. Wakamkalipia. "jamani nyamaza" lakini Bartimayo hakuwaskiza na akaendelea kumuita Yesu. Yesu akamskia na kusema, "Mleteni kwangu" umati ukasema "changamka, anakuita". Bartimayo akatupa koti lake akanyanyuka na kwenda kwa Yesu.'unataka nini?' Yesu akamuuliza. Bartimayo akamjibu 'nataka kuona" Yesu akamjibu, "Imani yako imekuponya." Bartimayo alikuwa na Imani Yesu alikuwa na uwezo wa kuponya watu. Unaweza kufikiria furaha Bartimayo alihisi alipoweza kuona? Pia fikiria alivyohisi alipofungua macho yake na kumuona Yesu.Hakuwa alivyokuwa tena. Alianza kumfuata Yesu akiwaambia watu kuhusu matendo mema aliyofanya.



## UNAWEZA KUFANYA?

- Angaza maombi yako kwa vitu vitakavyo mpendeza Yesu.
- Omba katika jina la Yesu kwa hekima na muongozo.
- Omba katika jina la Yesu kwa uponyaji na nguvu.
- Amini moyoni mwako kuwa kuna nguvu katika jina la Yesu.

# Mamlaka

## UCHEZE!

### "Sawa Kocha!"

1. Waeleze wachezaji wewe ndo kocha wa mchezo na utashindana na wachezaji katika huu mchezo.

2. Wachezaji wanasimama bega kwa bega katika mistari miwili wakiangaliana-ikiwa karibu kiasi unaweza kumgusa mwenzako ukinyoosha mkono. Mchezaji mmoja kwa wakati atakimbia kutoka mbele ya mstari hadi mwisho katikati ya mikono iliyinyooshwa

3. Unadhani ni rahisi? Mchezaji atakimbia amefungwa macho (na kitambaa, au soksi tatu zimefungwa pamoja au aambiwe afunge macho yake)

4. MUHIMU KWA KOCHA: Kocha mmoja atasimama mwisho wa mstari kuwasimamisha wachezaji wakimaliza. Ni jukumu la kocha kuimarisha usalama wa wachezaji

5. MUHIMU KWA WACHEZAJI: Waeleze wachezaji waliosimama kwenye mstari waelewe kama mchezaji anayekimbia akitoka kwenye mipaka kwa utaratibu wamuongoze na mikono yao wamrudishe kwenye mstari.

6. Mchezaji mmoja anachagulia kwa wakati kukimbia katikati ya hiyo mistari miwili kuanzia mwanzo hadi mwisho

- **Ukweli na uhusiano na maisha: wachezaji walimskiza na kumtii kocha kwasababu walimuamini-sote tunawasikiza kocha wetu. Inapaswa waumini zaidi wamskize Yesu na kumuamini na kumtii kwa sababu ana mamlaka yote**

## MASWALI

1. Kwenye mchezo uliona ugumu wa kumuamini kocha wako alipokuambia kimbia ukiwa umefungwa macho? Mbona ulimskiza kocha, kwanini wanariadha wanawasikiza kocha wao? (kocha anauzoefu, kocha anataka nishinde, kocha anampangilio na ana maono mazuri)
2. Kwa kuwa Mungu aliumba vitu vyote na anamamlaka ya kila kitu na Yesu ni mwana wake, Mfalme wa wafalme, unadhani kuna nguvu kiasi gani tunapoomba katika jina la Yesu? (nguvu zote zinapatikana)
3. Mungu asante kumtuma Yesu duniani, asante unaniruhusu mmoja ya watoto wako kuomba katika jina la Yesu. Mungu nakuamini na kutegemea Roho mtakatifu aniongoze. Mungu utatumiaje maisha yangu kukutukuza?(tulia)Naomba kwa jina la Yesu

©2018 cha Agano la Maombi Kwa Watoto / Michezo iliyotolewa na GameLife77.com. Haki zote zimehifadhiwa.




## KAZI YA KARATASI

1. **Hongera! Umefika mstari wa mwisho wa maombi MAMLAKA Je, unaweza kuandika hapa chini?**

2. **Jaza mapengo.**

   **Wafilipi 2:9: Kwa sababu hiyo Mungu alimuinua ________________ na**

   **akampa________________ ambalo ni ________________majina yote.**

3. **Ukifikiria hadithi ya bibilia ya leo, unadhani kwanini Bartimayo aliponywa na Yesu? Kama Yesu alimskia Bartimayo, ataweza pia kuskia ombi lako? Na ikiwa Yesu atakuskia, atajibu maombi yako kama alivyomjibu Bartimayo? Jibu ni 'Ndiyo'! Unaweza kumuomba Mungu uponyaji, nguvu, kwa msaada wako au wenzako kwa sababu Mungu anaskia na kujibu maombi**

4. **MUDA WAKUJIBU:**

   **Tengeneza kisanduku cha nia za maombi. Unaweza kutumia sanduku yeyote, au ya viatu ya kiwango chochote. Unaweza kuipamba na karatasi ya kufungia zawadi, au ibandike vipambo ama tu uiandike SANDUKU LANGU LA MAOMBI. Andika nia zako kisha uziweke sandukuni na ukumbuke kuomba kila siku. Mungu anapojibu maombi yako hata hiyo andika na umshukuru kwa kusikiliza na kujibu maombi yako!**

# Mamlaka

## NI WIMBO WA RAP!

**Yesu ni jina kuu kuliko kila jina!**

**AMINA! AMINA!**

**Katika jina la Yesu tunapata ukweli na nguvu!**

**AMINA! AMINA!**

**Katika jina la Yesu tunapata uponyaji na nguvu!**

**AMINA! AMINA!**

**Katika jina la Yesu tunapata matumaini na furaha!**

**AMINA! AMINA!**

**Katika jina la Yesu tunapata neema na amani!**

**AMINA! AMINA!**


**Katika jina la yesu tunapata upendo wa kweli!**

**AMINA! AMINA!**

Mwalimu anaongoza kwa kusoma maneno ya rangi nyeusi kisha watoto watamjibu na maneno ya rangi ya samawati.Baadae wahimize darasa waandike muziki wa rap kama kikundi,wakiandika fikira zao kwenye ubao. Waangalie watakavyo kuwa na furaha wanapo imba walichoandika.

# Taarifa la Agano langu la maombi

| JINA | TAREHE |
| --- | --- |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |





©2018 The Prayer Covenant for Children. All rights reserved.







©2018 The Prayer Covenant for Children. All rights reserved.






©2018 The Prayer Covenant for Children. All rights reserved.






©2018 The Prayer Covenant for Children. All rights reserved.






©2018 The Prayer Covenant for Children. All rights reserved.







©2018 The Prayer Covenant for Children. All rights reserved.




©2018 The Prayer Covenant for Children. All rights reserved.






©2018 The Prayer Covenant for Children. All rights reserved.




©2018 The Prayer Covenant for Children. All rights reserved.








©2018 The Prayer Covenant for Children. All rights reserved.

# Uumbaji kwa Mwendo wa Kristo


Hapa kuna njia rahisi kuwaonyesha watoto ujumbe wa injili ukitumia ishara za mikono. Tafadhali fwatilia kila mchoro hapo chini na uone vile inafurahisha kuitazama na jamii na marafiki zako. Hiki ni kifaa kinachoandamana vizuri na maombi ya wafuasi. “Nitumie kwa utukufu wako na nialike wengine wakufuate”




1. Hapo mwanzoni Mungu aliuumba dunia usio na kasoro.




2. Dhambi ikaharibu ukamili wa dunia.




3. Adhabu ya dhambi ni mauti.




4. Mwana wa Mungu, Yesu akalipa adhabu ya dhambi.




5. Yesu tu ndiye aliyekua Mtu kamilifu.




6. Yesu alikufa.




7. Yesu alizikwa.




8. Yesu alifufuka toka mauti




9. Kwa sababu Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zetu.




10. Yesu sasa anakupa fursa ya uzima wa milele.



11. Ungependa zawadi hii?



12. kwa Imani muombe Mungu awe Mwokozi wako.





13. Kawatangazie wote habari njema.

©2018 The Prayer Covenant for Children/Creation to Christ Hand Motions provided by GameLife77.com and line drawings provided by One Hope. All rights reserved

## Rasilimali ya Agano la maombi la watoto

Nenda kwenye mitandao utazame mifano ya vitabu vyetu, kadi za maombi, vitabu vya kuchora rangi na kufundishwa bure mambo ya video za picha na sauti na rasilimali zingine mitandaoni.







**theprayercovenant.org/children**

**MAONO:** Kuona muamko wa ukuu wa Yesu Kristo duniani kwote.
**LENGO:** Kuwaongoza watoto na watu wazima kumfuata Yesu kupitia nguvu ya maombi.

**UNGANA NA UHARAKATI LEO:** Kwa maelezo zaidi temebelea theprayercovenant.org/children

